Jumapili Agosti 18, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581772

www.ippmedia.com

www.facebook.com/nipashetz

www.twitter.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

UKURASA 13



**BAROBARO WA NGUVU Hakosi mavazi haya.....**

**Makonda** ana kwa ana na Biteko, Aweso mradi wa maji bilioni 500/-

UKURASA WA 3



**Othman** ataja chanzo kupotea uoto wa asili Zanzibar

UKURASA WA 3

**Ulimkimbia** mume, unarudi unakuta nafasi ilishazibwa kitambo

UKURASA WA 11

RIPOTI MAALUM

# Wanafunzi walivyogeuza shule vituo vya wavuta bangi, ubakaji

UKURASA 4





## Samia aguswa na mnufaika mkopo wa elimu ya juu, aahidi makubwa

UK. 2




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa na viongozi wengine katika Mkutano wa 44 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), jijini Harare, nchini Zimbabwe jana. **PICHA: IKULU**

## CHADEMA yatoa neno Lissu kuwania urais

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA YATAKATA MICHUANO CAF** UK.24 **MAONI,** UK.6



Askari kutoka vyombo vya usalama, mkoani Mwanza, wakifanya mazoezi ya matembezi ya hiari katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Mwanza jana, kwa lengo la kudumisha ushirikiano baina yao, kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: PETER ADOLF WA JESHI LA POLISI**

# CHADEMA yatoa neno Lissu kuwania urais

**Na Romana Mallya**

WAKATI Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiweka wazi kwamba ameshaandika barua ya kusudio la kuwania urais, chama hicho kimesema uamuzi kuhusu suala hilo utatolewa na kikao cha Kamati Kuu.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alipotafutwa na mwandishi wa habari hii jana, alikiri kupokea barua hiyo. Alipoulizwa kama kuna wanachama wengine walioandika kuwania nafasi hiyo, alisema kwa mujibu wa taratibu za chama, wakishafanya hivyo, majina hupelekwa katika kikao cha Kamati Kuu.

Juzi, katika mahojiano maalum na chombo kimoja cha habari, Lissu alisisitiza kusudio lake la kuwania urais na kwamba tayari ameshakabidhi barua kwa Mnyika tangu Agosti 6, mwaka huu.

Mnyika katika ufafanuzi wake alisema: "Katibu Mkuu akishapokea taarifa hupeleka Kamati Kuu na kuwekwa utaratibu wa watu waliotia nia. Kwa sababu yeye (Lissu) ameshajitangaza kwenye vyombo vya habari, kama kuna wengine walioandika hii ni mpaka kamati kuu ipokee taarifa ya Katibu Mkuu."

Mnyika alisema awali Lissu alitangaza nia hiyo akiwa katika uwanja wa ndege na alikuwa hajaandika barua kwa chama.

Alisema baada ya pale ndipo alipoandika kwa Katibu Mkuu na kusisitiza kama chama kina mwongozo kuhusu taratibu za nafasi mbalimbali ikiwamo urais.

"Kwa mujibu wa mwongozo huo, kwa nafasi ya ugombea urais na uchaguzi wa ngazi ya kitaifa, watia nia wanaandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu na Katibu Mkuu anapeleka taarifa hizo katika Kikao cha Kamati Kuu ambacho ndicho kinaamua utaratibu unaofuata," alisema.

Mnyika alisema kwa mujibu wa mwongozo huo, kwa ngazi ya Rais na uchaguzi ngazi ya taifa, Katibu Mkuu akishapokea taarifa hupeleka Kamati Kuu na kuwekwa utaratibu wa watu waliotia nia.

Kupitia mahojiano maalum, Lissu aliweka wazi suala la kuandika barua hiyo kwenda kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA.

Alisema Mnyika ana barua yake ya kusudio lake la kugombea Urais na nyingine ya kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti CHADEMA.

"Kwa hiyo nikisema mimi ni mtia nia kwa mujibu wa katiba na kanuni za CHADEMA nitakuwa sahihi kabisa. Nani wengine kama wapo wanaoweza kusema kama mimi," alisema Lissu.

Katika mahojiano hayo alikanusha madai ya kuwapo kwa mgawanyiko wa baadhi ya viongozi ndani ya chama chao, akisema kuwa ni joto la uchaguzi na kelele zilizoko ni za kawaida kabisa.

Akizungumzia mchango wa Sh. milioni 5.3 uliotolewa na viongozi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya matengenezo ya gari lake, Lissu alisisitiza kwamba haoni shida yoyote kuchangiwa na wanachama wa chama tawala kwa sababu, tangu harambee hiyo ianze hawakukuweka masharti ya watu wa kuwachangia.

Agosti 14, mwaka huu, Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, aliendesha harambee ya kumchangia Lissu ili kutengeneza gari lake, ambalo tangu akabidhiwe na Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma baada ya tukio lake la kushambuliwa kwa risasi, wadau mbalimbali wamejitokeza kufanya hivyo.

Harambee hiyo ilifanyika katika Uwanja wa Furahisha, jijini Mwanza katika mkutano wa hadhara wa Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ambapo Sh. milioni 5.3 zilipatikana.

**UTEUZI VIONGOZI KANDA**

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje CHADEMA, John Mrema, ilisema chama hicho kimefanya uteuzi wa makatibu wa kanda nne ambazo ni Magharibi, Serengeti, Victoria na Nyasa.

Alisema Kanda ya Magharibi aliyeteuliwa ni Meshack Buhahagare ambaye kabla ya uteuzi huo, alikuwa Ofisa Mwandamizi Makao Makuu. Grace Shio ameteuliwa kuwa Katibu wa Kanda ya Nyasa ambaye awali alikuwa Mweka Hazina wa Kanda hiyo.

Jackson Mnyawami, ameteuliwa katika Kanda ya Serengeti akiendelea na wadhifa huo Kanda ya Victoria ameteuliwa Zacharia Obed ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Katibu wa Kanda hiyo.

Mrema alisema uteuzi huo umethibitishwa na Kamati Kuu ya CHADEMA iliyoketi katika kikao chake cha kawaida Agosti 8, mwaka huu, Dar es Salaam.

# Rais Samia aguswa na mnufaika wa mkopo elimu ya juu, aahidi makubwa

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameguswa na maisha ya mwanafunzi Sylvester Masaki, ambaye ni mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu ngazi ya stashahada katika Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi Benjamin Mkapa (BMH).

Kutokana na kuguswa huko, Rais Samia ameahidi kuhakikisha vijana wengi zaidi kunufaika na mikopo hiyo.

Mwanafunzi huo ambaye analelewa na mama yake baada ya baba yake kufariki dunia akiwa na umri wa miezi sita, katika kutimiza ndoto ya kusoma diploma ya radiolojia, anasimulia namna alivyokuwa miongoni mwa wanufaika wa mikopo hiyo.

Majukumu ya mtaalamu wa radiolojia ni kugundua magonjwa: wanaradiolojia wanachambua picha za eksirei, CT-Scan, MRI, na Ultrasound kugundua magonjwa na hali mbalimbali za kiafya.

Katika ukurasa wake wa Instagram juzi, Rais Samia ameweka video fupi ambayo mwanafunzi huyo anasimulia namna alivyokuwa miongoni mwa wanafunzi wanufaika wa mkopo.

Mwanafunzi huyo anaeleza kuwa, "Nilikuwa ninatafuta chuo na kufikiria cha kusoma, mimi na wenzangu tulikuwa tunataka tusome mambo ya afya.

"Nikaangalia nikaona nikasome radiology. Nikasikia tangazo la mkopo. Kwa kawaida mkopo mnufaika ni mwanafunzi, lakini kwangu mimi imekuwa tofauti kidogo mnufaika ni mimi, pia na mzazi wangu.

"Nilipopata mkopo tangu hapo nimesahau mara ya mwisho ni lini nilimpigia simu (mama) kumwomba fedha za mahitaji," alisimulia mnufaika huyo.

Mama mzazi wa kijana huyo, Mary Msamwela, amemshukuru Rais Samia na kumpongeza kwa kuliona hilo kwa sababu mpango huo umewapunguzia wanawake wenzake mzigo wa kutafuta ada ya mtoto na fedha za matibabu.

"Tunashukuru sana Rais. Tunaomba aendelee kutoa mikopo kwa watoto wote wenye sifa za kupewa mikopo," alisema.

Kutokana na hilo, Rais Samia kupitia ukurasa wake ameandika kuwa, "Nimeutazama ujumbe wa Sylvester na mama yake kuhusu uamuzi wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa aina yake vyuoni unavyogusa maelfu ya familia na kuandika historia mpya.

"Maelekezo na mwongozo wangu ni kuhakikisha mpango huu unaendelea kwa ufanisi na vijana wengi zaidi wanufaika nao. Nakutakia kila la kheri Sylvester ma wenzako wote katika vyuo mbalimbali nchini," alisema.

Katika mwaka wa fedha 2024/25, serikali imetenga Sh. bilioni 787 kwa ajili ya mikopo na ruzuku kwa jumla ya wanafunzi 250,000, idadi hiyo imeongezeka kutoka wanafunzi 224,056 mwaka 2023/2024, hivyo kufanya ongezeko la jumla ya wanafunzi takribani 25.944.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kuchimba kisima cha maji safi, katika kitongoji cha Stooni, kijiji cha Nyichoka, wilayani Serengeti mkoani Mara mwishoni mwa wiki. Mradi huo, unasimamia Uhifadhi na Urejeshi Bonde la Mto Grumeti katika Ikolojia ya Serengeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Othman ataja chanzo kupotea uoto wa asili visiwani Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema uoto wa miti ya matunda na misitu ya asili katika visiwa vya Zanzibar unaendelea kupotea kutokana na jamii kuacha utamaduni wa urithi wa wazee wa kupanda na kuitunza.

Othman aliyasema hayo huko Kituo cha Maonesho ya Biashara Nyamanzi Wilaya ya Magharibi B, wakati wa uzinduzi rasmi wa Programu ya Kitaifa ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani kwa wananchi.

Programu hiyo ina lengo la kurejesha utamaduni wa kupanda na kutunza miti ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda, uoteshaji na uhifadhi wa misitu, miti ya kivuli na mbao.

Alisema serikali ilianzisha jitihada mbalimbali za kuifanya Zanzibar kuwa ya kijani tangu mwaka 1964 ikiwamo upandaji wa miti ya mipira, minazi sambamba na uhamasishaji wa wananchi kuendelea na kilimo cha viungo na kutunga sera na sheria mbalimbali ili kusaidia kulinda na kuhifadhi ukijani wa Zanzibar.

Pamoja na jitihada hizo kuendelea, alisema uoto na ukijani wa asili Zanzibar unaendelea kupotea kutokana na jamii kuwa na tabia ya kukata miti waliyoikuta ambayo wazee waliotangulia walifanya jitihada kubwa ya kuipanda, kuitunza na kuienzi.

Othman alisema kutokana hali hiyo, serikali imeanzisha mpango huo wa kitaifa ili kurejesha utamaduni kwa jamii kupenda kupanda na kuitunza miti ambao utakuwa shirikishi kwa taasisi, majeshi, wanafunzi, vikosi mbalimbali na mashirika yasiyo ya kiserikali kila mmoja kuhakikisha anatimiza wajibu wa kuirithisha Zanzibar kuwa ya kijani.

Pia alisema juhudi hizo pia zinakusudia kuwaleta pamoja wadau kutoka sekta na ngazi tofauti baada ya kuona kwamba yako mambo mengi yanayosababisha upoteaji mkubwa wa miti na misitu kutokana na sababu za kibinaadamu ikiwamo ukuaji wa miji na ardhi kubwa kutumika kwa ujenzi wa nyumba za makazi ya watu.

Alibainisha kuwa upoteaji zaidi wa miti na misitu uko zaidi katika ukanda wa magharibi wa visiwa vyote vya Unguja na Pemba kutokana na maeneo hayo kuwa na ardhi yenye rutuba na vyanzo vingi vya maji.

Othman pia alisema tatizo la ukataji wa miti na misitu pia limechangia ongezeko la athari za mazingira Zanzibar zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi na upotevu wa baioanuai.

Alisema mpango huo wa taifa umeanzishwa kwa nia ya kuhamasisha na kuwezesha wananchi wa Zanzibar na wadau wengine kuelewa umuhimu wa misitu, kuhifadhi miti iliyopo na kupanda miti kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

Makamu wa Kwanza wa Rais aliwataka wananchi wote, wafanyabiashara, wawekezaji, vikosi vya ulinzi na usalama, wanafunzi na mwananchi moja mmoja kushiriki katika utekelezaji wa mpango huo muhimu kwa Zanzibar.

Alisema mpango huo ni muhimu kwa vile utasaidia Zanzibar kupunguza kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi pamoja na hasara zingine zinazotokana na uharibifu wa mazingira.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, alisema kwamba mpango huo ni muhimu kwa vile kijani ya Zanzibar imepotea licha kwamba ni muhimu kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Alisema kutokana na hali ya ukame baadhi ya matiafa duniani hivi sasa yamekuwa yakipata shida kutokana na ongezeko la joto lililosababishwa na kukosekana miti kwenye nchi hizo.

Naye Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alisema kwamba wizara yake ni miongoni mwa wanufaika wa kwanza wa mradi huo kutokana na uzinduzi kufanywa katika eneo la maonesho ya biashara Zanzibar na kupandwa miti 150 ya aina mbalimbali kwenye eneo hilo.

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Iliyasi Pakacha Haji, alisema mpango huo utaibadili jamii ya Zanzibar kuwa na mitazamo kwamba miti na misitu inapaswa kutunzwa kuirithisha jamii ya sasa naya baadae.

Alisema mikakati mbalimbali shirikishi ya wadau mbalimbali inakusudiwa kutumika katika kufanikisha utekelezaji wa mpango huo na kwamba inakusudiwa kila mwaka miti 3,000 inapandwa kwenye maeneo mbalimbali.

## Makonda sasa uso kwa uso Biteko, Aweso

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amepanga kukutana na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kujadiliana kuhusu gharama kubwa za uendeshaji wa mradi wa maji wa Sh bilioni 500 unaotekelezwa jijini Arusha.

Makonda aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa kikao kazi na maofisa wa Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) kilichokuwa na mambo matatu ambayo ni hali ya upatikanaji wa maji, namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hasa kipindi cha kiangazi na kutokuwa na maji ya kutosheleza kunakosababisha kuwepo kwa mgao.

Makonda amewaomba wananchi wa mkoa wa Arusha wawe wavumilivu kwa kuwa anatafuta suluhu ya kudumu ya mradi huo wa maji.

"Hili jambo lazima tulikalie kikao na tulitafutie ufumbuzi wa haraka kwa kukubaliana kwa pamoja tuiombe Wizara ituingize kwenye watoa huduma na tutoke kwenye uniti moja ya watu wa viwandani kuja kwenye uniti moja ya watu wa makazini ili kusaidia kupunguza mzigo wa uendeshaji wa mradi huu," alisema.

Makonda aliwataka wataalamu mbalimbali ndani ya mkoa wa Arusha kuongeza umakini kwenye usimamizi wa miradi haswa katika hatua za awali za usanifu ili kutokuwa na miradi isiyotekelezeka na yenye gharama kubwa za uendeshaji suala ambalo limekuwa likiwaumiza walengwa wa miradi hiyo ya maendeleo. "Nitaomba kukutana na viongozi hawa ili kujadili kwa kina mradi huu na wapi tuelekee maana hali ya upatikanaji wa maji katika mkoa huu na maeneo mengine si nzuri lakini je changamoto za mabadiliko ya tabia nchi tunayachukuliaje na je vyanzo vyetu vya maji vinahimili mabadiliko hayo na je mpango wa taasisi husika yani nyie mmejipangaje? alihoji Makonda.

"Lakini ukosefu wa maji ya kujitosheleza upoje hali inayosababisha wananchi kuishi kwenye mgao huku hela zimetolewa na je Sh. bilioni 500 zilizotolewa zimeleta tija gani kwa wananchi hawa wa mkoa wa Arusha," alisisitiza.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa (AUWSA), Mhandisi Justine Rujomba, alisema wizi wa maji na mita za maji ni changamoto kubwa inayodumaza upatikanaji wa maji safi na salama kwenye jiji hilo haswa kwa watu wenye pesa na sio maskini kama inavyodhaniwa na wengi.

"Wanaoiba maji wale wenye pesa, tunawakamata wanaiba maji kasumba ya watu wenye hela hawapendi kulipa maji kutokana na taratibu za serikali zilizowekwa"

RIPOTI MAALUM

# Wanafunzi walivyogeuza shule vituo vya wavuta bangi, ubakaji

**Na Vitus Audax**

WAKATI serikali na wadau mbalimbali wakiongeza kasi kuboresha sekta ya elimu, hali imebainika kuwa tofauti kwa wanafunzi wa baadhi ya shule nchini.

Kuporomoka kwa maadili miongoni mwa wanafunzi, kumezidi kukua kila uchao ikiwamo kuiga mambo yasiyofaa katika jamii kama ulawiti, uvutaji bangi, ubakaji na ukabaji shuleni. Hali kama hiyo imebainika katika shule za sekondari Nyasho na Mwisenge zilizoko Manispaa ya Musoma mkoani Mara.

Vijana wa kiume wamekuwa wakiunda makundi ya uhalifu na kuteka wanafunzi wenzao huku wakiwafanyia ukatili hali ambayo imesababisha kifo cha mwanafunzi Said Yusufu (17) baada ya kupigwa na tofali kichwani.

Wanafunzi hao, kwa mujibu wa uchunguzi, wamekuwa wakijihusisha pia na unyang'anyi wa kutumia silaha kama bisibisi, ulawiti kwa wanafunzi wenzao, kujeruhi na kutishia walimu. Hali hiyo imeelezwa kuwakosesha amani walimu katika shule hizo.

Uchunguzi pia umebaini wasichana nao wametajwa kuunda vikundi vinavyojihusisha na vitendo vya ngono katika maeneo mbalimbali kwa kuvipa majina kama Vikoba, Amazon Group na Six Dadaz.

Kuwapo kwa hali hiyo kumezua taharuki katika shule hizo, hivyo kuifanya Shule ya Sekondari Nyasho kuitisha mkutano wa wazazi, uliohusisha bodi ya shule sambamba na viongozi wa ulinzi na usalama ngazi ya wilaya ili kupata suluhu ya tatizo hilo.

Mambo mengi yalijadiliwa katika kikao na kukubaliana kuwaondoa wanafunzi tisa ambao walibainika kuwa vinara katika matukio hayo. Wanafunzi hao walituhumiwa kuhusika kwenye mauaji ya mwanafunzi Yusufu.

Baadhi ya wazazi, akiwamo Robert Manyerere, wakizungumza katika kikao hicho, waliomba serikali na uongozi wa shule kuwafukuza wote waliohusika katika vitendo vya uhalifu badala ya kuzungumza na wazazi wao.

"Msije mkafukuza wengine halafu wakabaki watekaji, nao waende. Msiseme wale tumewafukuza lakini hawa watekaji wanaotembea na visu na mapanga tutakaa na wazazi pembeni. Wakiendelea kubaki hapa, sisi wazazi tunaohitaji elimu bora tuko tayari kuwahamisha wanafunzi wetu ili mbaki na hao wanafunzi wenu," alisema Manyerere.

**MATOKEO YA MITIHANI**

Mkuu wa Shule hiyo, Kitosy Francis, alisema katika matokeo ya mwaka 2023, wanafunzi 102 walipata sifuri huku akisema hali hiyo kuwa inatishia maendeleo ya elimu katika shule hiyo. Aliahidi kufanyia kazi ipasavyo maoni ya wazazi kuhusu wanafunzi watovu wa nidhamu shuleni hapo.

"Tutamtendea haki kila mwanafunzi atakayeonekana kuhusika katika vitendo hivyo kwa kumfukuza. Niwaombe wazazi mtupe ushirikiano kwani hatupo hapa kwa ajili ya kufukuza bali kujenga kizazi cha baadaye ili tupate viongozi wazuri hapo baadaye," alisema.

Francis alisema miongoni mwa mikakati inayofanywa na shule hiyo katika kurejesha nidhamu ndani ya mwezi mmoja ni pamoja na kuondoa wanafunzi tisa waliobainika kuhusika na makosa ya uhalifu



Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwisenge, Theopister Mashaur

na utovu wa nidhamu. Alisema alipofika shuleni hapo alikuta vikao vya bodi vinajadili kuhusu makosa yao ikiwamo kifo cha mwanafunzi.

Hali hiyo pia iko katika Shule ya Sekondari Mwisenge ambako katika kipindi cha miaka mitatu, wanafunzi 36 wamefukuzwa shule. Kwa mwaka huu pekee, wakifukuzwa wanafunzi tisa kwa makosa ya uvutaji bangi, kujihusisha na ushoga na makundi ya uhalifu.

Mkuu wa Polisi Wilaya (OCS) ya Musoma (OCD), Edson Mwamafupa, akizungumza katika kikao hicho, alithibitisha kupokea malalamiko kuhusu matukio ya uhalifu kutoka shuleni hapo pamoja na kushuhudia baadhi ya wanafunzi wa kiume wakijihusisha na ushoga mitaani.

"Ni kweli hata jana saa 7:00 usiku tumekamata mwanafunzi wa miaka 14 amemlawiti mtoto wa miaka minne. Kwa wiki hii pekee, tuna matukio yasiyopungua matano ya kulawitiwa kati ya hayo, manne ni ya watoto wa kiume na moja wa kike," alisema Mwamafupa.

Matukio mengi hasa ya ulawiti, alisema yamekuwa yakiripotiwa polisi na walimu lakini wazazi wamekuwa nyuma katika kufuatilia watoto wao na kwamnba mara chache wamekuwa wakifika wakati walimu wameshamaliza kazi hali inayoonesha wanawatupia mzigo wa malezi walimu.

Pia alisema matukio ya kutembea mitaani na visu, nondo na mimba za utotoni yamekuwapo hali inayochangiwa na wazazi kutokufuatilia nyendo za watoto wao.

Akithibitisha uwapo wa vitendo vya ushoga katika shule ya Mwisenge, OCD Mwamafupa alikiri na kusema mwanafunzi mmoja alikutwa akijihusisha na vitendo hivyo.

"Akitembea ni kama mwanamke, kabadilika kabisa hadi kuongea kwake ni kama mwanamke na usiku yuko mtaani. Ametoka mahabusu amedhaminiwa na mashtaka yake tunayaandaa tutampeleka mahakamani. Katika hilo hatuna namna kwa sababu imethibitika analawitiwa.

"Baada ya kupata dhamana siku moja nimekutana naye mtaani usiku kama saa 8:00 katika barabara ya Serengeti. Nilimhoji kama mwanafunzi anafanya nini akanijibu kama mwanamke akisema na wewe huku umefuata nini. Wewe eneo lako la kujitamba ni kituo cha polisi huku tuachie sisi," alisema Mwamafupa.

Mkuu wa Shule ya Mwienge, Theopister Mashauri, anasema: "Nyumbani wanatoka vizuri hasa mabinti lakini wanaishia mitaani. Kwanza wanafanya mapenzi alafu ndipo wanaibukia shuleni, wengine wanajiweka vimada wakati wa likizo."

Pia alitaja vitendo vya uvutaji wa bangi kuwa tatizo lingine shuleni hapo. Alisema wanafunzi wanafika tayari wamelewa bangi na kuleta vurugu kwa walimu wanaotekeleza wajibu wao.

"Hata wazazi ukiwashirikisha mwitikio wao unakuwa mdogo. Wakati mwingine wanakataa kuwa watoto wao hawavuti bangi lakini sisi walimu ndio tunakaa nao na tunawajua vizuri," alisema.

Kuhusu wanafunzi wanaojihusisha na vitendo vya ushoga, alisema wamewabaini na kuwafikisha kwenye vyombo vya usalama na malezi ili kuwasaidia.

**KILIO CHA WANAFUNZI**

Wakizungumza hivi karibuni na kituo cha ITV baadhi ya wanafunzi wa shuleni hapo wanaodaiwa kufanyiwa ukatili na baadhi ya wanafunzi wakorofi wa shuleni hapo, walisema hali hiyo imekithiri na kuwaogopesha kuendelea na masomo.

Mwanafunzi aliyetobolewa kiganja, Masuguliko, alisema wakati akitoka kwenye mtihani, alikutana na vijana wakimwambia anatafutwa na mmoja wa vijana hao wakorofi. Hakujali na kuendelea kujisomea ndipo walipofika vijana watatu akiwamo yule aliyedaiwa alikuwa akimtafuta.

"Alianza kunihoji kwa nini nilimpeleka Mwalimu nyumbani kwao, nikamwambia alinitaka nifanye hivyo ili akaongee na wazazi wako, kwa hiyo sikuwa na uwezo wa kumkatalia.

"Waanza kunikaba na kunipiga na kunibana wakihitaji kunichoma jichoni. Wakati nikijitetea, nikaweka mkono jichoni nikawa nimetobolewa kiganjani na kutokea upande wa pili. Niipiga kelele wakakimbia. Nilipotaka kuwakimbiza alifika mwalimu na kunizuia na kunipeleka kupatiwa huduma," alisema mwanafunzi huyo huku akionesha mkono uliojeruhiwa.

Alisema chanzo cha mwalimu huyo kutaka kwenda kwa wazazi wake ni kutokana na ukorofi uliopitiliza wa uvutaji bangi na uvamizi.

Wanafunzi wengine waliopitia madhira yanayosababishwa na wanafunzi hao walisema: "Matukio shuleni ni mengi ukiwemo uvutaji bangi, umalaya, ulawiti na hata utekaji. Ilikuwa siku ya Ijumaa tukiwa darasani, aliingia mwanafunzi akidai anatafuta madaftari yake yaliyopotea. Akaanza kukagua kila mwanafunzi akakuta rafiki yangu akiwa na madaftari mapya akadai ndiyo yake na kuyachukua akimwonya kutokusema kwa mwalimu wala wazazi," alisema mwanafunzi mmoja.

Alisema baada ya kuondoka kijana huyo, mwanafunzi aliyeporwa madaftari alikwenda kutoa taarifa kwa mwalimu lakini hakumpa ushirikiano wa kuogopa kuingilia vijana hao huku akiitaja kesi hiyo kuwa ya kipumbavu.

Mwanafunzi mwingine wa shule hiyo (jina limehifadhiwa) alisema vijana hao wamekuwa wakiwalazimisha wanafunzi kufanya ngono darasani na wakati mwingine kuwalazimisha kuwaingilia kinyume cha maumbile.

"Wakiwakuta wanafunzi wa kike huwalazimisha kwa kutaka wakafanyie chooni au bafuni," alisema.

Mmoja wa Wanafunzi waliojikuta wanaingia katika vitendo vya ushoga (jina limehifadhiwa) alisema: "Mwanafunzi jirani yetu kuna siku nilikuwa kwao akanilazimisha kwa kunivua nguo. Nilivyokataa akanilazimisha na kufanya hivyo kwa nguvu."

**WAZAZI WAFUNGUKA**

Mmoja wa wazazi wa watoto waliofanyiwa vitendo vya ukuatili shuleni (jina linahifadhiwa), alisema: "Nilimkuta nyumbani mwanangu amelala mapema, kumuuliza tatizo ni nini akaniambia nimepigwa na wanafunzi. Nilipomuuliza kama ametoa taarifa kwa mwalimu alisema ndiyo lakini mwalimu alimtaka kesho yake aoneshe waliompiga."

Alisema kesho yake wakati akienda kutoa taarifa ya wanafunzi hao, alizuiwa na wanafunzi wenzake kuwa vijana hao wangemfanyia kitu kibaya wakati wa kurejea nyumbani.

Baba wa Mwanafunzi aliyechomwa na kitu chenye ncha kali kiganjani, alisema alipokea taarifa hizo akiwa katika shughuli zake za kila siku na kukuta tayari mtoto alishatolewa hospitalini.

"Tulianza kuwatafuta waliomchoma tukabaini mmoja wao ambaye pia ana historia ya kufanya matukio makubwa na kisha mzazi wake kumsafirisha hadi tukio husika likisahaulika, hata hivyo kijana huyo alitukimbia," alisema.

Mzazi mwingine, Aisha Mwinyi alisema hali katika shule hiyo imesababisha watoto wao kuomba kuhamishwa shuleni kutokana na kunyanyaswa na kunyang'anywa mabegi yao ya shule. Pia alisema wanafunzi hao wamekuwa wakiwashambulia wanafunzi wenzao wanaoonekana kuwa karibu na walimu hao.

**WAZAZI HAWAJUI**

Baadhi ya wazazi wa wanafunzi wanaodaiwa kufanya vitendo hivyo dhidi ya wenzao, akiwamo Zainab Shaban, wakizungumza katika kikao cha wazazi na viongozi, walidai kutokujua nyendo hizo na kuwa hutoka nyumbani vizuri kwenda shuleni na kupewa huduma zote zinazohitajika.

"Huyu wa kwangu hajawahi kutembea kwa mguu wakati wa kuja shuleni. Huwa najitahidi kumpa hela ya usafiri labda tu wakati wa kurudi nyumbani. Lengo ni kumwezesha kufika shuleni mapema. Nilipofika hapa nimekutana na taarifa hizi, namuuliza umejiunga na vikosi gani anadai hajawahi kuwa kwenye vikundi," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyasho, Alfred Makunja, alilaani vitendo hivyo na kutaja hali hiyo kuwa si kwa shule hiyo pekee bali kwa shule nyingi za sekondari zinazoendekeza vitendo hivyo vinavyohatari maendeleo ya elimu,

**KAULI YA SERIKALI**

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Khalfan Haule, alionesha kushtuhwa na hali hiyo na kueleza kuwa nidhamu imeshuka kwa wanafunzi. Alisema serikali wilayani humo imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwashirikisha wazazi, walimu na wanafunzi wenyewe kuwa karibu zaidi ili kuhakikisha wanafunzi wanatumia muda wao vyema katika masomo.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Msoma, Bosco Ndunguru, licha ya kukiri kuwapo kwa vitendo hivyo, alisema wanaendelea na uchunguzi kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na dawati la ustawi wa jamii.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaahidi huduma bora mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu,** MADABA

LICHA ya wilaya ya Madaba mkoani Ruvuma kuwa na maeneo yenye milima na mabonde yanayosababisha maeneo ya bondeni kukosa huduma za mawasiliano, serikali imeahidi kuhakikisha inapata huduma bora za mawasiliano ili wananchi washiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi, wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha cha Maweso akiwa katika ziara ya kukagua hali ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika vijiji tisa vya wilaya hiyo.

Mahundi ametembelea vijiji vya Igawisenga, Wino, Maweso, Mwande, Matetereka, Mkongotema, Lutukira, Ndelenyuma, Gumbiro na Mbangamawe na kuzungumza na wananchi na kupata mrejesho wa hali ya huduma za habari na mawasiliano.

"Tunatambua jiografia ya Wilaya yenu ni ya milima na mabonde lakini serikali itahakikisha Madaba yote inapata huduma bora za mawasiliano ili mshiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali," alisisitiza.

Mhandisi Mahundi alitaja jitihada ambazo serikali inaendelea kufanya ili kuboresha huduma za mawasiliano katika wilaya ya Madaba kuwa ni pamoja na ujenzi wa minara mipya ya mawasiliano.

Alitaja jitihada zingine kuwa ni kuboresha teknolojia ya minara iliyopo na kuongeza vifaa kwenye kituo cha Mkongo wa Taifa cha Madaba ili kukiongezea nguvu ya kuwezesha huduma za uhakika za mawasiliano.

Philemon Machaine, akimwakilisha Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Wizara hiyo, alisema serikali kwa kushirikiana na watoa huduma, itaendelea kuboresha huduma za mawasiliano,ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watoa huduma wanaweka nishati ya umeme kwenye miradi ya mawasiliano inayotumia nishati ya jua ili mawasiliano yawe ya uhakika.

Katika ziara hiyo, Mhandisi Mahundi pia aliambatana na Mhandisi Shirikisho Mpunji kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Zablon Magabula, Mwakilishi wa Meneja wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) mkoa wa Ruvuma.

Mhandisi Mahundi alitumia fursa hiyo kuwahamasisha wananchi kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu, na kutoa rai kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi. Naibu Waziri Mahundi pia aliwataka wanaume kuwaunga mkono wanawake watakaojitokeza kugombea nafasi za uongozi.



Diwani wa Kata ya Endiamtu, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Lucas Zacharia akielezea mafanikio yaliyofanyika kwenye kipindi chake cha miaka minne wakati wa mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, eneo la uwanja wa getini, katika Mji mdogo wa Mirerani, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

# Sangu asisitiza mafunzo uongozi kwa bodi za mashirika ya umma

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, ameitaka Taasisi ya Uongozi kuweka kipaumbele katika mafunzo yanayohusisha wajumbe wa bodi mbalimbali za mashirika ya umma.

Amesema lengo ni kujenga uelewa mpana wa masuala ya kiuongozi ili wanapofanya uamuzi wowote wazingatie maslahi mapana ya taifa.

Sangu aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipofanya ziara ya kujifunza namna taasisi hiyo inavyofanya kazi na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi.

"Nimefarijika sana kusikia kuwa Taasisi ya Uongozi inatoa mafunzo mahususi ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji viongozi mbalimbali ndani na nje ya Tanzania ikiwa pia ni sehemu ya utekelezaji wa jitihada za kuimarisha utawala bora," alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anafanya jitihada za kujenga nchi katika nyanja mbalimbali, hivyo hawana budi kumuunga mkono kwa kufanya mafunzo ambayo yanaweza kuwafanya viongozi mbalimbali kuwa wazalendo na wenye kiu ya kuona taifa linapata maendeleo.

Sangu aliwasisitiza watumishi wa taasisi hiyo kuendelea na mshikamano katika kutekeleza majukumu yao, kwa kuwa jukumu la kutoa mafunzo kwa viongozi ni kubwa na linahitaji mshikamano.

Alisema amefanya ziara katika Taasisi ya Uongozi kwa kwa lengo la kujifunza kuhusu majukumu yake ambayo ipo chini ya ofisi anayoiongoza.

## Ziara ya ACT yaibua mazito

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema baada ya ziara yake katika mikoa 22, kimebaini mambo makubwa manne yanayowatesa wananchi ni pamoja na hali ngumu ya wananchi, vitisho na ubabe wa viongozi.

Makamu Mwenyekiti Bara wa chama hicho, Isihaka Mchinjita, aliyasema hayo jana Tanga Mjini, wakati wa kuhitimisha awamu ya kwanza ya ziara ya viongozi wakuu katika mikoa 22 na majimbo 125, ikilenga kuzindua kampeni ya kusajili wanachama milioni 10 kwa miezi 10.

Mchinjita alisema katika ziara hiyo, wamebaini changamoto ya uporaji na migogoro ya ardhi katika kila kona ya nchi ambako wananchi wamelalamikia suala hilo.

"Tumekutana na malalamiko ya wananchi kuporwa ardhi na serikali kupitia taasisi zake au kuwapa wawekezaji na kuna baadhi wanalalamikia migogoro ya wakulima na wafugaji kutokana na uzembe wa viongozi," alisema.

Pia alisema wamekutana na vitisho na ubabe wa viongozi kwa wananchi ambapo wananchi wameeleza kutishwa wanapotoa maoni yao.

"Tumekuta matukio ya kupotea na kutekwa kwa wananchi, manyanyaso kutoka kwa polisi na vyombo vingine. Malalamiko ya wananchi kuhusu huduma za afya wakizilalamikia ni mbaya, gharama kubwa za afya na vitendo vya ukatili vya wahudhumu wa afya," alisema.

Pia alisema wananchi wanalalamikia kuwapo kwa hali ngumu ya maisha, kupanda kwa bei za bidhaa kama vile mbolea, mafuta ya kula na petroli, dizeli, nauli za basi na kuongeza kwa kodi, ushuru, tozo na kuchangia ugumu wa maisha.

Pia alisema wananchi wanalalamikia ukosefu wa ajira na mazingira magumu ya kujipatia kipato.

Jambo lingine linalolalamikiwa alilitaja ni kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuwa wanufaika wanalia kuwapo kwa utaratibu mbovu wenye ubaguzi, usiotabirika na kufanyishwa kazi ngumu kama masharti ya kupatiwa fedha hizo.

Kuhusu matukio ya hivi karibu ya viongozi wa vyama vya upinzani kukamatwa na majaribio ya kuzuia mikutano ya vyama hivyo, Mchinjita alisema ni ishara mbaya kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alisema kuwa linahitaji mshikamano wa vyama vyote vya upinzani kukataa hali hiyo.

"Wito wangu kwa viongozi wenzangu wa upinzani, wapenda demokrasia na wananchi kwa ujumla ni kuwa matukio haya yanaonesha kuwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni ile ile.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu zaidi inatakiwa kuhusu mfumo vyama vingi vya siasa

**NI** katribani miaka 22 sasa tangu Tanzania ilipoingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Muda huo ni mwingi kwa kuwa kama ni mtoto, tangu kuzaliwa kwake atakuwa katika ngazi ya elimu ya chuo kikuu na hata wengine kuwa na familia kulingana na sheria za nchi.

Katika kipindi chote hicho, Watanzania wamepita mito, milima na mabonde hadi kufikia hatua ya sasa ya ustawi wa demokrasia kupitia mfumo wa vyama vingi vya siasa. Wako walioumizwa kwa sababu ya kuwapo kwa mfumo huo na wengine kufurahi na kunufaika kwa sababu mbalimbali.

Muda wote huo, imeshuhudiwa watu wakipata uhuru wa kukusanyika, kuzungumza mambo yao ikiwamo kuikosoa serikali huku vyombo vya habari vikipewa nafasi ya kuhabarisha umma kuhusu mambo yanayoendelea ndani na nje ya nchi. Demokrasia, utawala bora na utawala wa sheria vimeshamiri kwa kiasi kikubwa licha ya kwamba katika moja ya awamu za serikali, kulikuwa na manung'uniko kwamba uhuru wa mikusanyiko, demokrasia na habari viliminywa.

Pia kwa nyakati mbalimbali, ilishuhudiwa kuwapo kwa mivutano baina ya vyama vya upinzani na vyombo vya dola wakati wa kutaka kufanya mikutano ya ndani au ya hadhara. Jeshi la Polisi lililopewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao, ikiwamo kusimamia ulinzi na usalama wakati wa mikusanyiko hiyo, lilipiga marufuku baadhi ya mikutano huku likitoa sababu kwamba ni kutokana na taarifa za kiintelejensia na uwapo wa dalili za uvunjifu wa amani.

Matokeo yake, baadhi ya vyama vilipinga sababu hiyo na kuendelea na shughuli zao hali iliyosababisha baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa na wafuasi wao walikamatwa na kuwekwa ndani kisha kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Wengine walipata ulemavu kwa kuumizwa hata kupoteza maisha kwa kile kilichodaiwa kupinga amri halali ya Jeshi la Polisi.

Pamoja na hayo yote, ilifika wakati pia viongozi na wafuasi wa chama tawala - Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wale wa upinzani kupitia Chama Cha Wananchi (CUF) visiwani Zanzibar, walifikia hatua ya kutoshirikiana hata katika masuala ya kijamii kutokana na uhasama uliokuwa umekithiri baina yao. Hata hivyo, ulifanyika mwafaka na hatimaye kuanza kushirikiana pamoja na kuwa na mabadiliko ya katiba inayoruhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Pamoja na hayo yote, viongozi hawa walio katika utawala, wamekuwa wakisisitiza kuwa kuwapo kwa siasa za upinzani si chuki wala uhasama bali ni kuruhusu mawazo mbadala katika kuleta mustakabali chanya wa taifa. Pia imekuwa ikisisitizwa kuwa chini ya mfumo wa vyama vingi, watu wanatakiwa kupingana bila kupigana na kila mmoja akiheshimu imani na itikadi ya mtu mwingine.

Yote hayo, kiuhalisia, yako kinadharia zaidi. Hiyo ni kutokana na kauli na matendo ya viongozi na wafuasi wa vyama vya siasa wawapo majukwaani au wanapozungumza na vyombo vya habari. Wapinzani wamekuwa wakionekana kuwa maadui na upande wengine wanaohama kutoka chama kimoja kwenda kingine wamekuwa wakiitwa kwa majina mbalimbali kama vile makapi au wasaliti!

Siku chache zilizopita, kwa mfano, CCM Mwanza walimchangia Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, Sh. milioni 5.3 kwa ajili ya matengenezo ya gari lake ambalo liliharibiwa wakati aliposhambuliwa na watu wasiojulikana mwaka 2017 jijini Dodoma. Hali hiyo imezua minong'ono miongoni mwa viongozi na wafuasi wa vyama hivyo kwa nini imekuwa hivyo.

Mambo hayo yote yanayotokea na yanayoendelea, ni ishara kwamba elimu na uelewa kuhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa bado havijawaingia Watanzania wengi. Watanzania hawana budi kufahamu kwamba siasa si uhasama bali ni kuleta mawazo na fikra anuai katika kujenga Tanzania iliyo bora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamii ibadilike, kujichukulia sheria mkononi hakufai

**DODOMA** kunani? Ni miaka minane sasa tangu watafiti wawili na dereva wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Selian (SARI) Arusha wauawe na kuchomwa moto, katika kijiji cha Iringa Mvumi, Chamwino mkoani Dodoma.

Tukio hilo lilitokea mwaka 2016, chanzo kikidaiwa kuwa ni mmoja wa wanakijiji kupiga yowe kuwafahamisha wananchi wenzake kwamba ameona watu anaohisi ni wanyonya damu (mumiani).

Ikiwa ni miaka minane tangu kutokea kwa tukio hilo, lingine linalofanana na hilo la kujichukulia sheria mkononi, limetokea tena mkoani humo Agosti 10 mwaka huu, na kusababisha watu wawili kupoteza maisha.

Katika tukio la mwaka 2016, wataalamu hao wa kilimo walikuwa wakitafiti udongo, wananchi wakawahisi kuwa ni wanyonya damu, wakawavamia na kuwakata kwa mapanga na kuwachoma moto hadi kufa.

Watafiti hao walifika kijijini hapo kwa ajili ya shughuli hiyo, wakiwa hawajatoa taarifa katika ofisi ya serikali ya kijiji, wakiwa wanatafuta njia ya kutokea wakafika mahali wakakuta kinamama wakamwita mmoja wao.

Lengo la kumwita mmoja wa kinamama hao ilikuwa kutaka wamuulizie njia, lakini akawa anaogopa kwa kudhani kuwa walikuwa wanyonya damu, ndipo akapiga yowe ambayo ilisikika kijijini.

Nimejaribu kukumbushia kwa kifupi tukio hilo la kusikitisha, lakini sasa ninarejea kwenye lengo langu ambalo ni kuzungumzia tukio lingine linalofanana na hilo lililotokea tena mkoani humo.

Safari hii ni kwa wa kitongoji cha Juhudi katika Kijiji cha Ibihwa wilayani Bahi. Wananchi wamejichukulia sheria mkononi na kuwasababishia umauti wakazi wawili wa jijini Dodoma.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Anania Amo, amekaririwa na vyombo vya habari akithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba lililotokea Agosti 10, mwaka huu.

Kwa mujinu wa Kamanda Amo, waliouawa na wananchi hao ni Franco Mtasoka (29) mkazi wa Kisasa jijini Dodoma na Ramadhani Abeid (27) ambao walishambuliwa sehemu mbalimbali za miili yao kisha kuchomwa moto ndani ya gari lao.

Inasemekana kuwa baada ya wananchi kuona gari la watu ambao hawakuwafahamu wakiwa wamekaa kwa muda mrefu eneo la wazi kwenye nguzo za umeme, ndipo walipoamua kuwashambulia. Wananchi hao waliwatilia shaka kutokana na kipindi hiki kuwapo na matukio ya wizi wa watoto na kwamba hawakuwa na imani nao na kuanza kuwashambulia hadi kuwaua.

Lakini swali langu ni kwamba hivi kumtilia mtu shaka adhabu ni kuondoa uhai wake? Wananchi wanashindwa nini kuwakamata watu hao na kuwafikisha kwa viongozi wa serikali ili wakuchukuliwe hatua?

Ninaamini kuwa katika mazingira hayo, kuna nafasi ya kutosha kuzungumza na watuhumiwa ili kupata ukweli kuliko mwenendo huo wa kujichukulia sheria na kuondoa uhai wa binadamu wenzao.

Binafsi ninajua kuwa jamii iapomtilia mtu mashaka, inatoa taarifa kwa viongozi wa kitongoji, kijiji, mtaa au kwingineko ili hatua zaidi zichukuliwe, lakini hilo halifanyiki, matokeo yake ni watu kuuawa.

Hata akihojiwa na kukutwa ana kosa, hakuna mwenye haki kumwua. Badala yake, apelekwe kwenye vyombo vya sheria ili hatua zaidi dhidi yake zichukuliwe. Hivyo, mtindo unaotumiwa na baadhi ya wananchi anapaswa kulaanikiwa na kila anayethamini uhai wa mwenzake.

Mtindo wa kujichukulia sheria mkononi na kukatisha uhai wa wengine ni hatari inayoweza kuongeza chuki kwenye jamii na hata kusababisha matukio mengine makubwa ya aina hiyo.

Suala la utii wa sheria ni jukumu la kila mtu, lakini pia ni takwa la kisheria kwa kila mwananchi kuheshimu sheria za nchi katika nyanja zote kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Wataalam wa sheria wanasema, uvunjaji wa sheria na kujichukulia sheria mkononi ni kosa linalostahili adhabu kali, hivyo ingekuwa vyema kama kila mmoja ataachana na mtindo huo ulioshamiri ndani ya jamii.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Kongole Profesa Kabudi je, utaruhusu ubatili huu wa Katiba na sheria zetu ?



Pascal Mayalla

UTEUZI wa Prof. Palamagamba Kabudi ambaye ni bingwa wa katiba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa mara ya pili, uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, una maslahi makubwa sana kwa taifa hili lililojaa wanasheria mbalimbali wa katiba kuanzia serikalini, bungeni hadi mahakamani ambao baadhi yao wamekuwa chanzo cha uwapo wa sheria batili, zinazokinzana na Katiba ambayo ndiyo sheria mama.

Japo uteuzi huu umefanywa na Rais Samia kama unavyofanyika uteuzi mwingine wowote, kuna uwezekano Rais Samia ameongozwa na Roho wa Mungu, kumteua tena Prof. Kabudi aliyemtengua bila kutoa sababu alipofanya hivyo. Hii ni mara ya tatu kwa Prof. Kabudi kuongoza wizara hiyo, mara ya kwanza ikiwa baada ya kuteuliwa na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli.

Kwa vile Prof. Kabudi ni mwalimu wa sheria somo la katiba, kazi yake wizarani hapo si tu kutekeleza majukumu ya uwaziri bali atawafundisha sheria na katiba , wabunge na mhimili wa mahakama. Kwa mtazamo wangu, mmoja wa wanafunzi wake namba moja atakuwa Rais Samia mwenyewe kwa kumweleza ukweli kuwa Katiba yetu ina ubatili uliochomekewa kiubatili na pia sheria mpya ya uchaguzi ni batili, kwa ubatili huo huo ambao ulikwishabatilishwa na Mahakama Kuu.

Mimi pia nilisomea sheria na kutunukiwa shahada ya kwanza ya sheria (LLB) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na kupita mikononi mwa Prof. Kabudi. Wakati nikiwa mikononi mwake mpaka ninamaliza, kuna vitu sikuvifahamu kumhusu Prof. Kabudi lakini mwaka 2011 wakati UDSM inaadhimisha miaka 50 (Diamond Jubilee) tangu kuanzishwa kwake, mwanazuoni huyo mbobezi alitunukiwa tuzo ya 'outstanding GPA'.

Kwa muda wote wa miaka 50 ya UDSM, rekodi ya wastani wa daraja la ufaulu (GPA) ya Prof. Kabudi ya alama 4.9 haukuwahi kuvunjwa mpaka wakati huo wala sikuwahi kusikia kama kuna mwanafunzi mwingine yeyote ameifikia baada ya hapo. Kwa hiyo kuna uwezekano Prof. Kabudi ni mmoja wa wanazuoni mahiri na nguli waliobobea tulio nao kwa sasa katika sheria.

Serikali inafanya kazi kwa mtindo wa uwajibikaji wa pamoja (collective responsibility). Hata kama jambo fulani haliko sawa, walio wengi wanakubaliana nalo. Ukiona jambo hilo haliko sawa na hukubaliani nalo, kanuni ya uwajibikaji wa pamoja inakutaka ukae kimya.

Kwa vile yeye ni bingwa wa masuala ya Katiba na katiba ndiyo Biblia yetu na Msahafu wetu, tunamwomba asikubali Katiba yetu inajisiwe na wanasheria wababaishaji wa serikalini, bungeni na mahakamani ili kutunza heshima yake kuliko kukubaliana na uwajibikaji wa pamoja wa kututungia sheria batili. Ni bora akajiweka pembeni kuliko kuunyamazia ubatili huu wa ajabu wa Katiba yetu unaofanywa na wanasheria mguli wabobezi na wabobevu lakini wanatia shaka katika ubobebu na unguli wao.

Prof. Kabudi ni mwalimu wa somo la katiba pale UDSM na amefundisha mamia ya wanafunzi. Kanuni kuu ya katiba inasema Katiba ndiyo sheria mama, hivyo sheria nyingine yoyote itakayokwenda kinyume cha Katiba ni batili. Prof. Kabudi asiache huu ubatili wa Katiba yetu na ubatili wa sheria zetu uendelee chini yake.

Aidha, Prof. Kabudi ni miongoni mwa wale ma- 'Amicus Curiae' (marafiki wa mahakama) watatu wa ile kesi ya Mtikila ambayo Mahakama Kuu ilitoa hukumu kuhusu ubatili kwa Katiba yetu kunajisiwa na sheria batili ya uchaguzi inayokwenda kinyume cha Katiba.

Ushauri wao ni Mahakama isiliingilie Bunge kwenye utungaji wa sheria lakini anajua kuwa Bunge letu lilitunga sheria batili, likafanya mabadiliko batili ya Katiba, likauchomekea ubatili huo ndani ya Katiba yetu kiubatili.

Mahakama Kuu ikaamuru huo ni ubatili, mabadiliko ya Katiba ni batili na sheria hiyo pia ni batili lakini kwa heshima ya Bunge, kwa vile ni Bunge ndilo lililofanya ubatili huo, Mahakama ya Rufani ikajizima data na kusema: "the Court is not the custodians of the will of the people." Kwa tafsiri isiyo rasmi, Mahakama si mtunzaji wa matakwa na utashi wa jamii, mtunzaji wake ni Bunge kwa sababu ndilo linawawakilisha wananchi.

Mahakama ya Rufani ikalirudisha jambo hilo la ubatili wa Katiba na Ubatili wa Sheria kwa Bunge ndilo lirekebishe. Bunge letu mpaka sasa ninapoandika Makala hii, halikuwahi kuurebisha ubatili huo wa Katiba na ubatili huo wa sheria. Hii ina maana mpaka hii leo Tanzania tuna Katiba yenye ubatili na tuna sheria batili.

Naamini uteuzi huu wa Prof. Kabudi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria ni mpango wa Mungu kwa Tanzania, kumletea Rais Samia watu wenye uwezo watakaomwambia ukweli kuwa mambo mengi yamekuwa yakiikumba Tanzania kutokana na dhulma kubwa hii ya kupoka haki za Watanzania za kuchagua na kuchaguliwa kupitia kipengele batili ndani ya Katiba yetu na sheria zetu.

Swali ni, katika kipindi hiki Prof. kabudi atakuwa mkweli kutoka ndani ya nafsi yake?. Atamweleza Rais Samia ukweli kuhusu ubatili wa Katiba yetu na sheria yetu mpya ya uchaguzi ambayo yeye (Rais) ameitia saini hivi majuzi au atajizima tena data kama alivyojizima enzi za JPM kwa kutembelea kanuni ya uwajibikaji wa pamoja? Muda utasema,

Mungu Mbariki Prof. Kabudi kusimama kwenye kweli. Mungu Mbariki Rais Samia kukubali kuambiwa ukweli wa ubatili wa Katiba na sheria na kuufanyia kazi.

**Mungu Ibariki Tanzania**
**Paskali**
**+255 754 270403**

# BoT yasisitiza mjumuisho kifedha na teknolojia

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Mkurugenzi wa Ustawi na Fedha Jumuishi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Sadiki Nyanzowa, amesema kuna umuhimu wa mjumuisho wa kifedha na teknolojia mpya za malipo katika uchumi wa kidijitali ambao unaendelea kukua nchini.

Alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam katika jukwaa la Mastercard lililowakutanisha wadau muhimu katika tasnia ya teknolojia ya fedha ili kuangazia hali ya sekta na kukuza ushirikiano wenye matokeo chanya nchini.

Jukwaa hilo ni kielelezo cha dhamira ya Mastercard ya kuchangia katika ukuaji wa uchumi kupitia huduma bunifu za malipo ya kidijitali na ushirikiano wa kimkakati nchini Tanzania.

Alisema uchumi wa Tanzania umeonesha kuimarika, huku ukuaji halisi wa pato la taifa ukitarajiwa kufikia asilimia 5.7 katika mwaka wa fedha wa 2024/25.

Alisema pia Ripoti ya Benki ya Dunia inaonesha kuwa licha ya changamoto za kiuchumi duniani, sekta ya huduma, hususan huduma za kifedha na bima, imekuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi nchini.

Naye Rais wa Mastercard Afrika, Mark Elliott, alisema kampuni za teknolojia za kifedha zimeleta mageuzi kupitia huduma bunifu kama vile malipo kwa njia ya simu, uwekaji akiba kidijitali na miamala ya blockchain, pamoja na kukuza wigo wa huduma za kifedha na kuwawezesha wananchi wasiofikiwa na huduma za kibenki. Ushirikiano baina ya Mastercard na wadau, sambamba na maendeleo ya teknolojia ni muhimu katika kufanikisha mageuzi hayo. Hii itahakikisha usalama na ufanisi katika huduma za malipo na kukuza mjumuisho wa kifedha na ushirikishwaji wa Watanzania katika uchumi.

Katika jukwaa hilo, jopo la wataalamu wakiwamo viongozi wa taasisi za sekta binafsi na viongozi wa serikali walijadili mada kuhusu kuziba mapengo yaliyopo katika ushirikishwaji wa kifedha ili kufikia uwezeshaji wa kiuchumi.

"Jopo hilo lilijadili mchango wa teknolojia katika kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za kifedha. Mada zilizojadiliwa ni pamoja na mikakati ya kusaidia wajasiriamali, biashara ndogo na za kati (MSME), mipango ya pamoja, ubunifu katika huduma za kifedha kupitia simu za mkononi kwa jamii ambazo hazijafikiwa na huduma na mifumo ya udhibiti katika kukuza ujumuishaji.

Naye Makamu wa Rais Mwandamizi na Meneja wa Mastercard Afrika Mashariki, Visiwa vya Bahari ya Hindi, Shehryar Ali, alisisitiza umuhimu wa kukutanisha wadau katika jukwaa hilo ili kukuza ushirikiano na kuchangia katika maendeleo endelevu ya kiuchumi.

"Jukwaa hili ni hatua muhimu katika kujenga mfumo imara na jumuishi wa kifedha nchini Tanzania. Kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendeleza ushirikiano wa kimkakati, malengo yetu ni kujenga mfumo-ikolojia wa malipo ulio salama na unaoweza kuzifikia jamii ambazo hazijafikiwa na huduma za kibenki kote barani Afrika," alisema Ali.

Jukwaa la Wadau Tanzania liliandaliwa na Mastercard ni sehemu ya mikakati ya Mastercard ya kujenga mfumo salama na jumuishi wa kifedha nchini Tanzania.

# TBS yafungua mashindano tuzo za ubora

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limefungua mashindano ya tuzo za kitaifa awamu ya tano kwa mwaka 2024 ili kuwatambua na kuwapongeza watu binafsi waliotoa mchango katika kuboresha miundombinu ya ubora au taasisi zinazofanya vizuri.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Ashura Katunzi, alipozungumza na waandishi wa habari wakati akifungua mashindano hayo huku akibainisha kwamba yatahamasisha ubunifu na uboreshaji wa bidhaa na huduma zinazotolewa nchini kupitia taratibu zilizowekwa chini ya miundombinu ya ubora.

Pia alisema tuzo za ubora kwa awamu ya tano kwa mwaka 2024 zimeandaliwa kwenye vipengele vitano ambavyo ni kipengele cha tuzo kwa kampuni bora ya mwaka, tuzo kwa bidhaa bora ya mwaka, tuzo kwa huduma bora ya mwaka, tuzo kwa muuzaji bora wa bidhaa nje ya nchi na kipengele cha tano ni tuzo kwa mtu mmoja aliyefanya vizuri kwenye masuala ya ubora.

Alisema washindi wa tuzo za kitaifa awamu ya nne kwa mwaka 2023/2024 walishiriki katika mashindano ya tuzo za ubora kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Sahara (SADC) ambapo washiriki wa Tanzania walifanikiwa kupata ushindi katika vipengele vitatu.

"Washiriki wa Tanzania walifanikiwa kwenye mshindi wa pili wa SADC tuzo ya muuzaji bora wa bidhaa nje ya nchi (East Cost Oil and Fats Ltd), mshindi wa tatu kampuni ya bora ya mwaka ya SADC (Mjasiriamali)- CAPS Tanzania Ltd, mshindi wa tatu mota huduma bora wa SADC (Mjasiriamali)- CAPS Tanzania Ltd," alisema Dk. Katunzi.

Pamoja na hayo alisema kipengele cha kwanza hadi cha nne wameandaa tuzo kwenye makundi mawili kwa kila kipengele ambapo tuzo kwa kampuni kubwa na pia tuzo kwa kampuni ndogo au wajasiriamali wadogo na kwamba kipengele cha tano kinahusisha tuzo moja kwa mtu mmoja pekee

Hata hivyo, alisema maandalizi, usimamizi na tathimini ya tuzo hizi yanafanywa na kamati maalum ambayo inahusisha taasisi mbalimbali.

Alisema miongoni mwa vigezo vinavyotumika kuwapata washindi ni pamoja na nini kinafanywa na taasisi husika au mtu binafsi kuonesha ubora wa bidhaa, huduma, ufanisi katika uzalishaji au utendaji kazi kwa ujumla.

Dk. Katunzi alisema kigezo kingine ni pamoja na ni kiasi gani taasisi au mtu binafsi ameweza kunufaika kwa kuongeza ubora wa bidhaa, huduma au utendaji kazi na vilevile ni kwa namna gani biashara imekua baada ya kuboresha bidhaa, huduma au uzalishaji na utendaji kazi.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Mwendesha baiskeli ya magurudumu matatu maarufu Guta, akiitengeneza baada ya kuharibika katika barabara ya Kawawa, eneo la Magomeni Mikumi, Dar es Salaam, hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Mshindi wa kwanza wa kipengele kikuu wa droo ya kampeni ya 'Ni Balaa!', Bankason Yusuph (kulia), akiwa mwenye furaha wakati akikabidhi zawadi ya mfano wa hundi ya 20,000,000/- kutoka kwa Mkuu wa Vodacom Tanzania Plc Kanda ya Kaskazini, George Venant, jijini Arusha juzi. Yusuph, pia amepata fursa ya kuchagua shule ambayo kampuni hiyo, wataisaidia kukarabati maktaba ili kuboresha elimu ikiwa ni sehemu ya kuchangia maendeleo ya elimu nchini. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara, Peter Toima (kushoto), akimpongeza Diwani wa Kata ya Naisinyai wilayani Simanjiro, Taiko Kurian Laizer, baada ya kusimikwa kuwa kiongozi wa kimila wa jamii ya wafugaji (Laigwanani), katika sherehe zilizofanyika Kijiji cha Naepo, hivi karibuni. **PICHA: GIFT THADEY**




Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Andullah Said akizungumza na wamiliki na wakurugenzi wa shule binafsi, baada ya kufungua mafunzo ya utumiaji wa mfumo wa lipa ada kwa njia ya kidijitali, Mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**



Wachuuzi wa matunda wakiwa wameyaweka kwenye baiskeli zao, wakati wakisubiri wateja kando ya ukuta wa makaburi ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAISHA

AGOSTI 18, 2024
Nipashe Jumapili

Baba, Mama na Mwana




**BAROBARO WA NGUVU Hakosi mavazi haya.....**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Uwekezaji kwenye nyumba unalipa



Ukurasa 12

**HARUSI**




**TUMBO LINALOVUTIA**




Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | R | U | N | G | U |
| A | ■ | ■ | ■ | Y | ■ | N |
| J | ■ | D | A | U | ■ | G |
| E | D | A | ■ | K | U | U |
| S | ■ | I | N | A | ■ | Z |
| H | ■ | M | ■ | ■ | ■ | W |
| I | G | A | N | A | ■ | A |


### FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

FAA,NOA, RAI, IBA, IDAKE, TAIFA, FANYA, IMARA, ANDIKIA, USHINDI

### TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




@Msamba

### AMSHA AKILI




### CHEKA



Alichokifanya Adaktari

WATOTO wawili walikuwa wakitembea barabarani, mbele walimuona mwendesha pikipiki akihangaika kuwasha.

**Juma:** Habari kaka?

**Mwendesha pikipiki:** Safi tu.

**Juma:**Naona unaangaika na pikipiki tatizo nini?

**Mendesha pikipiki:** Napiga kiki kuwasha

**Juma:** Kwani Aziz Ki anatengeneza Honda?

**Mwendesha pikipiki:** Nyie watoto achene kunitania

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ulimkimbia mume, unarudi nafasi ilishazibwa kitambo!

***KARIBU tena msomaji wangu kwenye safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Ni mengi nayazungumza hapa kuhusu yanayojiri kwenye maisha yetu ya kila siku. Bila shaka yanakubariki na yapo unayojifunza kwa ajili yako na wengine wanaokuzunguka.***

Wiki iliyopita nijadili kwa nini majaribu ni sehemu ya maisha yako. Nikaelezea pamoja na mengine aina za majaribu na kwa nini yanatokea. Nikasema majaribu yanaweza kuwa na manufaa kwetu ingawa yanaonekana kutusababishia maumivu.

Ni muhimu kwa sababu yanaweza kutufanya pia tuwe wanyenyekevu na kutufundisha kusimama katika imani. Watu wengi wamekuwa na imani haba kiasi cha kufikia hatua kumkufuru Mungu wasijue kwamba majaribu ni sehemu ya maisha ili kuimarika zaidi kiimani

Kwa sababu shetani ni mshitaki wetu, Mungu huruhusu majaribu ili ujitafakari ulipoanguka. Lipo kosa unaloweza kulifanya, ukalijutia maisha yako yote. Tena unalifanya pale Mungu anapotaka kukupa muujiza wako.

Msomaji wangu, leo nikupe mfano wa mtu aliyeshindwa kuvumilia jaribu akajikuta anapoteza neema ambayo Mungu alimpa. Shetani alimpitia na kumuondoa kabisa kwenye nafasi yake na sasa anajuta!

> **Neno la Mungu linatuambia kwamba kile akitoacho mtu kinywani mwake ndicho kilichoujaza moyo wake. Akamwambia amechoka hawezi kuendelea kuishi maisha ya kutegemea sadaka za washarika kanisani.**

Namzungumzia mama mmoja, mke wa mtumishi katika kanisa moja. Ni familia yenye watoto na walianzia mbali kimaisha hadi kujikuta wakiwa na wito wa kumtumikia Mungu. Huduma yao imekuwa ikikua siku hadi siku.

Wiki iliyopita nilieleza jinsi shetani anavyowatenda wanadamu kwa akili. Nikasema kuwa zipo familia ambazo shetani amepata nafasi kuzishambulia na kusababisha maumivu yasiyoelezeka. Moja ni familia hii ninayojadili hapa.

Mke wa mchungaji huyu pengine kwa kuwasikiliza washauri wasiofaa akajikuta amejitoa kwenye nafasi yake. Mama huyu baada ya kujipanga sawa sawa akampasulia mume wake yaliyo moyoni mwake.

Neno la Mungu linatuambia kwamba kile akitoacho mtu kinywani mwake ndicho kilichoujaza moyo wake. Akamwambia amechoka hawezi kuendelea kuishi maisha ya kutegemea sadaka za washarika kanisani.

Mumewe akabaki amedukwaa akidhani ni utani kumbe mama alikuwa akimaanisha alichokisema. Mama akakusanya alichotaka akaondoka zake. Inasemekana yupo mtu alikuwa anamlaghai aachane na mume wake ili wakaishi pamoja amfungulie biashara zenye hela.

Mchungaji akaendelea na huduma kuifanya kazi ya Mungu kwa miaka kadhaa pasipo mke wake. Hata alipojaribu kuwasiliana naye arudi alikataa na mawasiliano yakakatika kabisa.

Mchungaji akaendelea na huduma pasipo mke. Upweke ukamshinda ikabidi atafute mwenza mwingine. Maisha yakaendelea, huduma ikazidi kukua, waumini wakaongezeka sana.

Yule mama huko alikoenda alichokitarajia kwamba atafanya biashara atakuwa na uchumi mzuri hakikutokea. Maisha yakawa magumu akatamani kurudi kwa mume wake.

Akajaribu kufuatilia kilichokuwa kinaendelea kwa mume wake wa awali. Akadokezwa kwamba mume anaye mwanamke mwingine. Akawaza kurudi nyumbani kwake.

Alipojaribu kuwasiliana na mumewe kumuomba arudi, mume akamwambia haitawezekana kwa sababu aliondoka mwenyewe, tena kwa jeuri na dharau kwamba hayawezi maisha yanayotegemea sadaka za kanisani.

Msomaji wangu, roho ya kuasi siku zote ina majuto. Na hasa kama ulipoondoka uliondoka kwa mbwembwe au hukutaka kusikia maonyo ya jamaa zako. Au unapoondoka ulionyesha dharau, ulitamka maneno ya kudhalilisha. Majuto hapo ni lazima.

Na hii ndio kazi ya shetani kuwatoa watu wazuri kwenye nafasi zao nzuri ili kuwapa majuto. Wanawake ndiyo walengwa wakuu wa shetani kuwaangamiza.

Huwajaza roho ya tamaa ili kuzikimbia familia zao na kuwaacha waume zao na watoto wakiwa bado wanawahitaji. Wapo wanawake wengi waliozikimbia familia zao lakini baadaye mambo yakawa sivyo wakarudi kwa aibu huku wamechoka kiafya.

Lakini, hata kama mwanamke umetelekeza ndoa yako kwa miaka mingi, rudi ukarekebishe. Hata ukikuta mwenzi wako tayari kashaendelea na maisha yake, kama mama niliyemjadili hapo juu, mwombe msamaha tu ili uwe na amani na furaha tena! Unahitaji kuwa huru, dhamiri yako inahitaji kuwa huru!

Msomaji wangu, mwanamke siku zote ni mlinzi wa mwanaume. Mungu ameweka wazi katika neno lake, Yeremia 31:22 "Hata lini utatanga-tanga, Ee binti mwenye kuasi? Kwa maana BWANA ameumba jambo jipya duniani; mwanamke atamlinda mwanaume".

Hivyo, mwanamke anapomkimbia mwanaume humuachia maumivu. Nyota ya mwanamke ina nguvu mara mbili ya mwanaume. Baada ya Ibrahim kumuoa Sara utajiri uliongezeka!

**Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Kuna kiwango cha maumivu hakipaswi ukae kimya

USIWAITE wenzako wavivu, wamepata nafasi waliyo nayo kwa kubahatisha. Usifanye hayo kwa sababu tu milango yako ya maisha katika kazi iliwahi kufunguliwa kabla yao.

Ndiyo. Usinipunguzie mwendo kwa sababu heshima na tamaa, havikai nyumba moja.

Ngoja nikuambie ukweli. Ukitaka kufikia mafanikio yako katika maisha na hata masuala ya uongozi, chagua moja.

Sijui unanielewa au niongeze sauti! Ni hivi, usihusudu, wala kuingiwa na tamaa na nyakati za watu.

Sikiliza ndugu yangu, jenga tabia ya kuheshimu nyakati za watu, kwa sababu nyakati huzunguka. Pale mahali hazina yako ilipo, ndipo moyo wako ulipo.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya haya ninayoyasema na uhusiano wako na Mungu, sasa sijui umeyaweka wapi?

Kama ndivyo basi ni muhimu tuheshimu nyakati za watu ili na wewe ujenge nafasi ya kuheshimiwa wakati wa nyakati zako.

Wako wanaodiriki kusema kama maisha ninayo, watoto ninao na mali ninazo, hivi nahitaji nini kingine? Wanasahau kuna nyakati Mungu aliyewatoa sehemu moja kwenda nyingine. Hawakumbuki ni yeye aliyewavusha.

Acha kiburi kaka acha kiburi dada! Ni wangapi waliotafuta mali na kujilimbikizia utajiri wa kukufuru; na leo wameshushwa vyeo kwa sababu walikutana kile kinachoitwa uteuzi na utenguzi?

Ubaya huwa haujifichi. Yaani huna tofauti na wale ndugu wanagombania, wanatesa watoto au familia ya mwenzie.

Unadiriki kusema hadharani tena kwa majigambo, haiishi mpaka iishe. Unakimbilia kupeleka kesi mahakamani ili nini? Vitu vya ulimwengu huu visikugombanishe.

Mara umenunua kiwanja una-post (unachapisha mtandaoni), unaanza kujenga una-post. Mwisho wa siku ujenzi unakwama!

Ndugu yangu, wakati mwingine hufanikiwi kwa sababu unatangaza ndoto zako kabla hazijawa! Usisahau si kila mtu anafurahia mafanikio yako.

Labda hujanielewa. Hizo ndoto zako za kutaka ukubwa, cheo na umaarufu hakuna tatizo.

Ni mfululizo wa picha, mawazo, mihemko na hisia ambazo hutokea akilini, kwa kawaida bila makusudi.

Mambo yote hayo huja katika hatua fulani fulani za usingizi; na wakati mwingine zikawa ni ndoto za mchana kweupe.

Usitangaze ndoto yako, tangaza matokeo, vinginevyo utaishia kuuzwa utumwani kama Yusufu. Yusuph akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia.

Aidha, historia isikuzuie kutimiza ndoto yako. Ni muhimu kuwa na utamaduni wa kuheshimu ndoto zetu hata kama tunadhani kuwa ni ndoto ndogo kama vile ndoto ya kumiliki aina fulani ya mali.

Wengi husema wanataka kutimiza ndoto zao, hata hivyo ni wachache hufanikiwa kutimiza ndoto zao.

Kwa kuwa binadamu tuna ndoto tofauti tofauti. Ni ngumu kuwa na kanuni moja ya jinsi ya kufikia ndoto zetu, hata hivyo uzoefu unaonyesha mambo kadhaa ambayo watu wengi waliofikia ndoto zao wamefanya.

Kuota ndoto ya mabadiliko ya maisha yako, sio tuu kuwaza au kutamani kufikia hali fulani, bali kuota kwa usahihi ni kutengeneza picha kichwani ya hali unayotaka kufikia, au mambo unayotaka kuyapata.

Mungu hawezi kukuacha ukafa bila kutimiza ndoto zako, utaona unapita kwenye misukosuko mingi lakini bado unaishi.

Wakati mwingine Mungu hutuma malaika waje wakusaidie bila wewe kujua.

Ni kama ule wakati wa Ibrahimu, alikuwa katika shida na mkewe Sarah. Alikuwa hana motto, malaika wakaja wakamwambia Sarah atapata mtoto ni kama kipindi cha Sodoma na Gomora, malaika wakaja wakamwokoa Lutu na familia yake.

Malaika akija katika ulimwengu wa mwili, yaani duniani anavaa mwili kama ulionao wewe; ndio maana kuna watu mmesaidiwa na watu msiowajua hata mkiwatafuta muwashukuru.

Hamtawaona tena hao walikuwa malaika na anaweza akaja akavaa mwili wa kidhaifu kabisa wala usimjue.

Wabaya wako ndio watakuwa viongozi wa kupiga kofi (kushangilia) kwenye mafanikio yako. Halafu iko siku moja, wabaya wako watafitinishana katika hila zao.

Cha ajabu ni kwamba inaweza ikatokea wewe ndio ukawa msuluhishi wao. Jambo la muhimu ni kwamba wachekee wabaya wako ili wasijue kama unajua ubaya wanaokufanyia.

Wengine waache walalamike. Hawalalamiki ili wasaidiwe namna ya kuishi. Wanalalamika angalau wasinyang'anywe haki yao.

■ ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI





Unaweza kusema ni moja ya harusi iliyotikisa 2024, wakati Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi alipomuoza binti yake na kuandaliwa sherehe ya kipekee iliyohudhuriwa na watu maarufu nchini wakiwamo viongozi serikalini na wastaafu. PICHA: MC Dr Cheni.











## MITINDO

# BAROBARO WA NGUVU Hakosi mavazi haya.....



KAMA wewe ni kijana barobaro ambaye unahamasika na mitindo ya mavazi, unatakiwa kufahamu kwamba unahitaji aina tofauti za suruali ambazo zitakuweka katika utanashati zaidi.

Aina hizi za suruali zitakupa nafasi pana ya kwenda sehemu mbalimbali ukiwa na mwonekano wa kupendeza.

**JEANS**

Vijana wengi wanapendeza zaidi kuvaa suruali za jeans, na kulifanya kuwa vazi pendwa kwa wanaume.

Kutokana na umuhimu wake, hutakiwi kukosa Jeans kwenye kabati lako la nguo, kama una uwezo wa kifedha nunua hata aina nne ya mitindo na rangi tofauti.

Jeans inayopendeza zaidi na vijana wengi wanavutiwa nayo ni 'slimfit jeans' ambayo inabana kiasi mwili.

**SWEAT PANTS**

Sweat pants ni suruali za pamba ambazo hazina mambo mengi, hupendeza zaidi kuvaliwa wakati ukiwa nyumbani au mazoezini.

**KADETI**

Kijana mara nyingi hakosi suruali za aina hii, wengi wanapenda kutokana na mitindo yake na urahisi wa kufua.

Ukivaa kadeti yako na shati hakuna shida kwani utaenda sehemu zote bila kukumbana na sheria za mavazi.

**SURUALI ZA VITAMBAA**

Wengi hawapendi kuvaa suruali za vitambaa, lakini aina hii ya nguo ni nzuri kutokana na kuwa laini.

Suruali hizi mara nyingi zinavaliwa na suti. Watu wanaogopa kuwa nazo kutokana na gharama kuwa kubwa, lakini ni nzuri kuwa nazo.





UREMBO

# TUMBO LINALOVUTIA

Na Mary Geofrey



MIAKA ya zamani kuwa na tumbo kubwa inafahamika kama kitambi, ilihusishwa na utajiri au uwapo wa mafanikio kwenye maisha.

Hata hivyo, mambo yamebadilika kwa sasa tumbo kubwa ni tatizo hususani kwa wanawake, kwani wengi wanaona sehemu ya kukosa mwonekano na kuharibu urembo.

Pia kwa upande wa wanaume, tumbo kubwa huondoa dhana nzima ya utanashati kwa sababu inazima mwonekano wa miraba ya kiume.

Tatizo hili husababishwa na aina za mafuta yanayokusanywa tumboni kwa wingi na kuwa chanzo cha magonjwa sugu.

Hizi ni baadhi ya hatua unazopaswa kuchukua ili kupunguza ukubwa wa tumbo.

**Chai ya rangi**

Chai ya rangi huwa na kemikali muhimu kwa kuunguza mafuta ya tumbo, huitwa epigallocatechin gallate.

Kemikali hizi kwa miaka mingi zimekuwa zinatumika katika kutengeneza vyakula na vinywaji kwa ajili ya watu wanaotaka kupunguza tumbo.

Ufanisi wake huongezeka zaidi kwa watu wanaofanya mazoezi, pia ikichanganywa na limao au ndimu.

**Apple cider vinegar**

Umewahi kwenda supermarket ukakutana na chupa imeandikwa kwa majina hayo?

Hiyo chupa ni chaguo sahihi kwa watu wenye tumbo kubwa.

Huwa na kemikali za acetic acid ambazo tafiti nyingi zinathibitisha uwezo wake wa kuunguza mafuta ya tumbo.

Kiasi cha vijiko viwili kwa siku vilivyo changanywa kwenye maji vinatosha kabisa kuleta majibu chanya.

**Usingizi**

Kulala muda mrefu ni afya, hakikisha unalala kwa saa 9 hadi 12 kwa siku ili kupunguza tumbo.

Usingizi ni dawa njema pia kwa afya ya mwili na akili, ukifanya hivyo utapunguza kitambi.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# CHAPATI YA NYAMA YA KUSAGA



PISHI hili linaweza kutumika kama sehemu ya kuongeza ubunifu kwenye biashara ya mgahawa au hoteli.

Ni kitafunwa kizuri kinachoweza kusindikizwa na juisi au chai.

Unga wa ngano una aina nyingi za mapishi. Achana na maandazi, chapati za maji, kalmati, mikate na chapati za kusukuma za kawaida unazokula kila siku.

**Maandalizi**

Hatua ya kwanza ni kuandaa nyama ya kusaga kwa kuiosha na kuikausha maji.

Osha hoho, karoti na kitunguu maji na ukate kate kwa saizi unayoipenda, kisha weka kwenye chombo kisafi kwa ajili ya kuvitumia wakati wa kuandaa chapati yako yenye nyama ndani.

Anza kupika nyama ya kusaga itakayochanganywa na ngano ili kutengeneza chapati yenye nyama ndani.

Bandika sufuria jikoni ongeza mafuta kiasi yakipata moto weka vitunguu maji, koroga mpaka viwe rangi ya kahawia.

Ongeza kitunguu swaumu kilichosagwa na ukoroge kwa dakika moja kisha weka nyama ya kusaga ikoroge vizuri kisha ufunike ichemke mpaka maji yaliyopo yakauke.

Nyama yako ikikauka maji ongeza chumvi, pilipili manga kijiko kimoja, masala kijiko kimoja na ukoroge vizuri.

Ongeza pilipili hoho na karoti, funika kwa dakika tano kisha nyama yako itakuwa tayari.

Tukishaandaa nyama ya kusaga sasa tuandae chapati kwa kuanza kukanda unga wa ngano ili kuondoa mabonge bonge ya unga na kuhakikisha unga ni msafi.

Andaa bakuli la kukandia kisha weka unga, ongeza chumvi robo kijiko na mafuta kiasi au siagi ya kukandia. Ongeza na maji kiasi kisha uanze kukanda.

Kanda unga wa chapati kwa dakika 15 au zaidi kwa kutegemea wingi wa unga.

Unga ukilainika ongeza mafuta ya kupikia vijiko viwili au siagi kisha ukande tena kwa dakika 3 ili unga uchanganyike vizuri na mafuta.

Unavyoweza kupika chapati za nyama ya kusaga zitakuwa tayari kwa kuliwa na kinywaji chochote.

Ugawe kwa kuukata madonge matano au sita kulingana na wingi wa unga wako na ufunike kwa dakika 10 au zaidi kabla ya kusukuma.

Chukua donge moja moja na usukume kutengeneza duara kisha weka nyama ya kusaga kiasi katikati na ulifunge duara kwa kulizungusha.

Rudia hatua hiyo kwa madonge mengine yaliyobakia kisha uanze kusukuma madonge uliyokwisha kuyafunga na nyama ndani.

Sukuma donge lako vizuri kupata chapati yenye muonekano mzuri, wengine hutengeneza chapati yenye pembe nne siyo lazima duara.

Ukisha sukuma vizuri washa jiko, andaa kikaangio kwa ajili ya kuchoma chapati zako mpaka ziive vizuri.

Rudia hatua hiyo kwenye maduara mengine yaliyobaki na chapati yako itakuwa tayari kwa kuliwa.

## DONDOO

Na Restuta James

# Tunza usafi wa nyumba kwa kuhifadhi vyakula kwa usafi

NYUMBA hata kama ikiwa haijakamilika kwa kiasi kikubwa, usafi unaipa thamani na mwonekano wa kipekee. Usafi unaozungumzwa ni ule wa mpangilio mahsusi wa vitu.

Mathalani, tumezoea nyumba nyingi kuwa na friji kwa ajili ya kuhifadhi vyakula vinavyoharibika kwa urahisi hususani vilivyopikwa, lakini ni watu wachache wanaozingatia mpangilio wa stoo au uhifadhi ya vyakula vingine.

Ester Donald ni mtaalamu wa mpangilio na mapambo ya ndani anaeleza kuwa vyakula kama viazi, vitunguu, maboga, matunda kama mapapai, mananasi na ndizi hasa kama yanaendelea kuiva, hayajazingatiwa sehemu za kuwekwa na badala yake mara nyingi ni vyakula vinavyowekwa chini.

“Kuweka vyakula hivi chini kunasababisha unadhifu wa nyumba usionekane. Hata kama uko kwenye nyumba ya kupanga na una nafasi ndogo, ukiweka vyakula vyako kwenye mpangilio kama inavyoonekana kwenye picha, utaifurahia zaidi nyumba,” anasema.

Anashauri kwamba zipo pia ‘storage’ za plastiki zinazouzwa kwenye maduka, japokuwa anashauri kwa mwenye uwezo kununua za mbao.

“Mbao inaongeza nakshi kuliko plastiki na chuma japokuwa kila mtu ana kitu anachopendelea katika hivyo. Kwangu mimi mbao ni nzuri zaidi kwa kuwa ina tabia ya kuongeza uhai kwa kuleta utulivu,” anasema Ester ambaye pia anatengeneza samani ndogo ndogo za ndani.

Anasema samani hizo ni vitu vinavyohamishika na hivyo kumpa urahisi mwenye nyumba kubadili mwonekano wakati wowote anaopenda.



## MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Uwekezaji kwenye nyumba unalipa





KATIKA maisha ya kila siku, watu wamekuwa na juhudi za kupata mafanikio katika nyanja mbalimbali ikiwamo uwekezaji katika vitegauchumi mbalimbali, ikiwamo ujenzi wa nyumba.

Uwekezaji ni mchakato mzima wa kuiweka mali katika mfumo maalumu wa kifedha kwa ajili ya tija zaidi ya baadaye ambayo inaweza kuongezeka au namna fulani yenye kuleta faida baada ya muda fulani.

Leonald Michal, ni mshauri wa masuala ya uwekezaji na anaelezea kanuni bora za kuwekeza kwa tija kupitia ujenzi na umiliki wa nyumba.

Anashauri kwamba unapowekeza kwenye ujenzi wa nyumba, miongoni wa mambo ya kuzingatia ni pamoja na unataka kujenga nini kulingana na mahitaji katika uhalisia wa sasa na wa baadaye.

“Unapaswa kutazama ni aina gani ya watu watakaotumia nyumba yako, shughuli gani ambazo zitakuwa zinafanyika katika nyumba husika.

“Kwa hiyo ni muhimu pia kushirikiana na mtaalamu aliyebobea katika usanifu. Pia kujenga kwa kuzidi uwezo wako huleta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi, sehemu nyingine kutotumika na kutokuwa na faida ya kutosha, kutumia pesa nyingi kwa kitu kisicho na faida na kuwa na gharama kubwa za uendeshaji wa jengo,” anashauri.

“Pia kujenga kwa kutokidhi mahitaji, husababisha hasara kwa kulazimika kufanya upanuzi wenye gharama kubwa zaidi, kuacha nyumba na kutafuta nyingine, kutoridhika na kutokuwa huru zaidi.


Ni muhimu kuhakikisha kwamba unachojenga kitaleta faida kwa kipindi hicho cha uwekezaji. “

Anashauri kwamba ni vyema kujiuliza maswali kama je, kodi ambayo wapangaji wanailipa inaleta faida, mtaji uliotumia kujengea utakuja kujilipa baada ya muda gani, faida ya kipesa itaanza kupatikana baada ya muda gani, na je nyumba yako itadumu kwa miaka mingapi?

Jambo lingine muhimu anasema unapowekeza katika sekta hiyo ya nyumba ni kufuata sheria na taratibu zote husika ili uwekezaji wako usibughudhiwe na mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuhatarisha mchakato wa kupata faida kwa kujenga katika eneo linaloruhusiwa kisheria na kwa kufuata sheria na taratibu zote.

Pia anashauri kwamba makadirio ya gharama za ujenzi yatakusaidia namna ya kujipanga juu ya mtaji wa kukuwezesha kusogeza mbele na kwamba si vyema kujenga kwa kubahatisha.

“Ni muhimu kuiona faida katika mipango yako ambayo umeifanya kabla ya kuanza ujenzi,” anasisitiza.




***KINYUNYIZO CHA LEO...** *HATA UMBEA NI KAZI JAPO HAUNA AJIRA...*

# Watu 18,000 waambukizwa ugonjwa Mpox barani Afrika

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

JUMLA ya visa 18,737 vya maambukizi ya virusi vya homa ya nyani vimeripotiwa barani Afrika tangu mwanzoni mwa mwaka huu.

Kulingana na Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa Afrika, (CDC), kufikia sasa, visa 3,101 vya maambukizi yaliyothibitishwa na visa 15,636 vinavyoshukiwa vimeripotiwa katika nchi 12 wanachama wa Umoja wa Afrika.

Ugonjwa huo umesababisha vifo vya watu 541, ikiwa ni asilimia 2.89 ya kiwango cha maambukizi.

Taarifa ya CDC , ilieleza visa zaidi vya maambukizi vimeripotiwa tangu mwanzo wa mwaka huu kuliko 2023, ambao ulioshuhudia visa 14,383.

Idadi hiyo ya maambukizi inajumuisha aina tatu ya virusi vya homa ya nyani, moja kati ya hizo ni kirusi kipya na hatari zaidi cha Clade 1b kinachoweza kuambukiza zaidi na kilichopelekea Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza dharura ya afya ya kimataifa, ikiwa ni tahadhari ya juu zaidi kutolewa na shirika hilo. **DW**

# Uganda imewarejesha polisi 100 Congo DRC

**KAMPALA,** Uganda

UGANDA imewarejesha polisi 100 wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) waliokimbia mapigano kati ya waasi wa M23 na jeshi la serikali ya nchi yao hivi karibuni.

Taarifa ya jeshi la Uganda ilisema baada ya kuthibitisha vitambulisho vya uraia, polisi hao waliruhusiwa kuingia Uganda kama kitendo cha kiutu na kulingana na sheria ya kimataifa.

Msemaji wa Jeshi, Meja Kiconco Tabaro, alisema polisi hao walirejeshwa pamoja na silaha zao na kuongeza kuwa wakimbizi wanaendelea kuingia Uganda wakikimbia machafuko yanayoendelea mashariki mwa nchi hiyo.

**Waasi wa M23 wameanzisha tena uasi katika eneo hilo lililozingirwa na makundi ya wanamgambo tangu mwaka 2022.**

Waasi wa M23 wameanzisha tena uasi katika eneo hilo lililozingirwa na makundi ya wanamgambo tangu mwaka 2022.

Juni, waasi wa M23 waliukamata mji wa Kanyabayonga, na kuutumia kama lango la kuingia kwenye miji mingine ya jimbo la Kivu Kaskazini.

Juhudi za jeshi la DRC kuwarejesha nyuma waasi ziliongezeka mwaka uliopita likitumia droni na ndege za kivita, ingawa waasi hao wamezidi kujiimarisha na kudhibiti maeneo mengi zaidi.

Mapigano katika jimbo la Kivu Kaskazini, yamesababisha zaidi ya watu milioni 1.7 kuyakimbia makazi yao, na kufanya jumla ya wakimbizi wa ndani kufikia milioni 7.2. **DW**



Wakimbizi wa Sudani kutoka jimbo la Sennar kusini-mashariki mwa Sudani wakiwa katika kambi maalumu wakikimbia mapigano yanayoendeshwa na vikosi vya RFS. **PICHA: AFP**

## Hamas yapinga mapendekezo kumaliza vita Ukanda wa Gaza

**GAZA,** Palestina

KUNDI la Hamas limesema limekataa marsharti mapya yaliopendekezwa na wasuluhishaji wakiongozwa na Marekani katika mazunguzmo yanayofanyika nchini Qatar.

Hadi kufikia jana, juhudi za kidiplomasia kupata suluhu ya kusitisha vita vilivyodumu kwa zaidi ya miezi 10 katika ukanda wa Gaza zimeonekana kutozaa matunda.

Licha ya hayo, Rais wa Marekani, Joe Biden kusisitiza kwamba baada ya mazungumzo hayo wapatanishi wanamatumaini ya kupatikana kwa suluhu.

Marekani imemtuma Waziri wake wa Mambo ya Kigeni Antony Blinken, kwenda nchini Israel kushinikiza wakubali mapendekezo yalioafikiwa hivi karibuni .

Wapatanishi kutoka mataifa ya Misri, Qatari na Marekani wanashinikiza utekelezwaji wa mapendekezo yaliowasilishwa na Rais Biden, ambayo yalipendekezwa na Israeli.

Katika taarifa ya pamoja, wapatanishi wa mzozo wa Gaza, walisema kwamba tayari wamewasilisha kwa pande zote mbili mapendekezo hayo hivi karibuni.

Hamas, ambayo haikutuma mwakilishi katika mazungumzo yaliyofanyika mjini Doha imepinga kile ambacho imetaja kama marsharti mapya kutoka kwa Israeli.

Waziri Mkuu wa Israeli Benjamin Netanyahu alitoa wito kwa wapatanishi kuishinikiza Hamas kukubali mapendekezo ya Rais Joe Biden. **RFI**

# Kamala azindua mpango wake kabambe kuiongoza Marekani

**CAROLINA,** Marekani

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, amezindua mpango wake wa uchumi ambao atautekeleza endapo atachaguliwa kuwa rais wa taifa hilo.

Harris juzi alikuwa North Carolina katika mwendelezo wa kampeni yake ya uchaguzi na kuzindua mpango huo wa uchumi na moja ya kipaumbele chake ni kujenga uwezo wa ununuzi wa Wamarekani.

Mpango huo uliobeba jina la kujenga uchumi wa fursa, utakuwa mwongozo wa mgombea huyo wa urais wa chama cha Democratic katika uchaguzi utakaofanyika Novemba 5, mwaka huu.

"Nitaweka juhudi zangu zote katika kutengeneza fursa kwa watu wa tabaka la kati, ili kuimarisha usalama wao wa kiuchumi, utulivu na utu. Kwa sababu ninaamini sana kwamba wakati tabaka la kati linapokuwa na nguvu, Marekani inakuwa na nguvu, alisema Harris.

Kufanya watu tabaka la kati kuwa kipaumbele tayari ulikuwa ujumbe wa Rais Joe Biden , lakini Kamala Harris anaongeza nguvu zaidi.

Aliahidi kutunza uchumi wa familia za raia wa Marekani ili kuboresha uwezo wao wa ununuzi.

"Sote tunajua kuwa bei iliongezeka wakati wa mlipuko wa UVIKO wakati mifumo ya usambazaji ilishindwa. Lakini leo hii sio kesi tena, na bei bado ni kubwa sana. Na hiyo si nzuri." Alisema.

Ili kutatua tatizo hilo, Harris alipendekeza mfumo unaonuiwa kuzuia ongezeko la matumizi mabaya ya bei za vyakula na mafuta.

Aliahidi kufutwa kwa deni la matibabu kwa mamilioni ya Wamarekani, mkopo wa ushuru wa dola 6,000 kwa kuzaliwa kwa mtoto au hata usaidizi wa dola 25,000 kwa ununuzi wa nyumba ya kwanza.

Kamala Harris pia ameahidi kupambana na mgogoro wa nyumba katika nchi ambayo kodi zinaendelea kuvunja rekodi kwa kupanda.

Nguvu ya ununuzi na mfumuko wa bei bado inaleta wasiwasi kwa Wamarekani wengi.

Hata hivyo, wengi wanaamini kama Kamala Harris ataweza kutekeleza mpango wake.

Haitoshi kupata ushindi kwenye uchaguzi wa urais,wanachama wa Democrat watalazimika kurejesha udhibiti wa Baraza la Wawakilishi pamoja na kuendelea kushikilia Bunge la Seneti.

**RFI**

## MAKALA

# MATOKEO YA TEUA TENGUA YA MARA KWA MARA



Na Magabilo Masambu

HIVI karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya uteuzi na utenguzi wa baadhi ya viongozi hasa katika Baraza la Mawaziri na wengine kuwabadilishia nafasi zao katika nafasi zingine. Kwanza, nakubali kwamba Rais anayo mamlaka na uhalali huo wa kutengua na kuteua kwa mujibu wa sheria, hivyo kutengua na kuteua si tatizo.

Kwa miaka ya hivi karibuni na hasa kuanzia awamu ya tano, tumekuwa tukishuhudia mabadiliko ya mara kwa mara tofauti na miaka au awamu zilizopita. Zamani ilikuwa kazi ngumu sana kusikia Baraza la Mawaziri limekuwa na mabadiliko hata katika nafasi zingine kama wakuu wa mikoa na wilaya. Ilikuwa nadra sana kusikia mkuu wa mkoa au wilaya fulani ametenguliwa, lakini hivi karibuni na sasa, limekuwa jambo la kawaida kabisa.

Natambua kwamba mabadiliko ya nafasi yoyote ile yanakuwa yamekusudia kuboresha ya utendaji pale anayewateua pamoja na vyombo vyake, wanapoona inafaa. Hata hivyo, mabadiliko haya pia yakiwa ya mara kwa mara, yanaibua maswali mengi kwa sisi tusiokuwa sehemu ya uamuzi kwamba kwa nini mara kwa mara.

Bahati mbaya Zaidi, wako baadhi ya viongozi ambao wanateuliwa kwenye nafasi ambazo wamewahi kutenguliwa. Sasa unajiuliza kwa wakati huo walionekana kutotosha katika nafasi hizo, mara sasa wanafaa tena katika nafasi zilezile! Inawezekana nyakati na watu wanabadilika na mabadiliko hayo wakati mwingine yanaweza kufanya viongozi wabadilike pia.

Leo nieleze mtazamo wangu juu ya tengua teua za mara kwa mara, ambao unaweza usiwe wa kila mtu na ikiwa hivyo ndivyo binadamu tulivyoumbwa. Hatujaumbwa kuyatazama mambo katika mtazamo mmoja.

Hii tengua teua ya mara kwa mara pamoja na uzuri wake, inaweza kusababisha mambo yafuatayo;-

Mosi, kuzuia kabisa ubunifu kwa viongozi katika nafasi zao mpya. Tengua teua inamfanya kiongozi kuwa na mawazo tegemezi kwenye mamlaka za uteuzi kwa maana kwamba kila atakalokuwa anafikiri kufanya katika ofisi, anakuwa na hofu nalo. Ikiwa litapendeza mamlaka za uteuzi au litawachukiza, hivyo itamlazimu kila mara kabla ya kulitekekeza, apate uhakika ikiwa halitawahudhi waliomteua. Hali hiyo itamfanya kiongozi huyu ndani ya ofisi yake mpya asifanye jambo jipya hata kama litakuwa na manufaa makubwa kwa ajili ya ofisi. Anakuwa na hofu ya kutenguliwa wakati wote.

Pili, tengua na teua za mara kwa mara zinaweza kusababisha viongozi kujipendekeza zaidi badala ya kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu na kanuni za kazi. Wakati wote wanakuwa wanatafuta njia ya kufurahisha mamlaka za uteuzi wakidhani kwamba wataepuka kutenguliwa. Kwa kufanya hivyo, wakati mwingine wanajikuta wanakosea zaidi na kufanya mambo yasiyofaa katika ofisi za umma na wakati mwingine kuudhi hata mamlaka zenyewe.

Tatu, wizi na ubadilifu. Ikiwa kiongozi ataingia kwenye nafasi ambayo anajua wakati wowote anaweza kutenguliwa, anaweza kufanya ufujaji wa kutisha ndani ya muda mfupi kuhofia kwamba akichelewa atajikuta akitenguliwa bila chochote. Kwa hiyo watendaji wanaweza kukiuka sheria na taratibu za kazi kwa kusaka fedha zaidi kuliko kuwatumikia wananchi.

Nne, ni kutojiamini. Ili kiongozi atekeleze mambo yake vizuri, lazima awe na utulivu wa moyo. Kama hajiamini hawezi kupata matokeo yake kwa kuwa kila atakalokuwa anajaribu kufanya, ataharibu kwa sababu hajiamini wakati wote. Hii inaweza kuwakuta hata washauri wa Rais na pengine ndiyo maana tunashuhudia mabadiliko ya mara kwa mara.

Tano, pengine laweza lisionekane kwa haraka ni juu ya magonjwa ya moyo, sukari na vidonda vya tumbo. Hii tengua teua inafanya viongozi wengi wasiwe watulivu na kuwa wenye mawazo wakati wote. Kila mara wakiona ile karatasi wanaita 'PDF' au 'Mkeka wa Mama' kama unavyoitwa, hata kama si ya uteuzi labda Rais anampongeza Rais wan chi fulani kwa kuchaguliwa na wananchi wake, tayari hofu.

Wengine wakiona huo mkeka, wanawaambia madereva wao wasome halafu watawaambia nini kimeandikwa. Mbaya zaidi, mkeka huo umekuwa ikitolewa usiku kwa hiyo wakati mwingi hawa viongozi hawalali usingizi wenye afya kila mara wanashinda mitandaoni wakichungulia kuona kama ile karatasi imetoka au la.

Ushauri wangu ni kwamba kwanza, sjajua zamani ilikuwaje watu walidumu kwenye nafasi zao kwa muda mrefu kuliko sasa. Lakini ninachopenda kushauri ni kwamba mamlaka zinazohusika na uteuzi lazima zifanye kazi ya kuchimba zaidi kabla ya kutoa mapendekezo nani anafaa nafasi fulani ili kuepuka kuwatoa watu kwenye nafasi fulani kisha kuwarejesha katika nafasi hizo hizo baada ya muda fulani.

Viongozi wanaoteuliwa wapewe uhuru mkubwa wa kutekeleza majukumu yao bila kudhani kwamba wanapotekeleza waliowateua wanawatazama hiyo inaweza kuwafanya wakosee hata katika mambo wanayoyajua vyema. Pia viongozi wa kisiasa ni muhimu kuzingatia sana ushauri wa wataalam na waweke mazingira ya kushauriwa hata katika mambo wasiyopenda kusikia bila kusababisha madhara yoyote kwa wanaowashuri.

Aidha, viongozi wa juu wawe makini sana na watu wanaojiita chawa au wale wanaowasifu kila mara. Wanaweza kuwa wanawapotosha kwa maslahi yao binafsi badala ya maslahi ya umma.

Mwisho, nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu wateule waliopata uteuzi katika nafasi zenu mpya.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Uzuri ni tabia, si urembo utembezwao*



Na Adam Fungamwango

POPOTE ambapo binadamu atakwenda, tabia njema ndiyo silaha yake ya kwanza na si vinginevyo.

Utakapokuwa na tabia njema inakuwa ni rahisi kupata marafiki, kujumuika na watu na wakakukubali, kiasi kwamba hata unapotaka kuondoka, wengine watasikitika, wapo watakaolia na wengine kukuombea dua kwenye maisha yako.

Binadamu wamegawanyika sehemu mbili. Wako wenye tabia ya wema, ucheshi na kujichanganya na watu popote wanapokwenda. Hawa wanajipatia marafiki kutokana na tabia yao.

Binadamu wenye tabia hii ni rahisi kuzoeleka na wamekuwa hawabagui watu, wataongea na kucheka na yeyote bila kujali wadhifa, cheo, pesa na muonekano. Anafanya hivyo bila hata kujali nini anaweza kukipata baadaye.

Lakini wako binadamu walijaaliwa kiburi, kujiona na kujimwambafai. Hawa popote anapokwenda anataka aonekana kuwa yeye ni mtu spesheli, siyo mtu wa mchezo mchezo, ni mwenye pesa na hana shida ndogo ndogo.

Ili aonekane hivyo ni lazima kwanza aringe, ajione yeye ndiyo yeye. Watu hawa hata salamu hawatoi kwa mtu tu hivi hivi. Huchagua mpaka mtu wa kusalimia. Akiona au kukuhisi ni kapuku na huwezi kumsaidia chochote katika maisha yake, hupati salamu yake na wala ukimsalimia wakati mwingine haitikii.

Hata baadhi ya kinadada hasa wakijifahamu kuwa ni warembo, yaani kajaliwa uzuri, basi huwa na tabia ya maringo na kujiona ni binadamu wa aina ya pekee ambaye anapaswa kunyenyekewa na si yeye kuongea vizuri na watu.

Huyu anaweza kukupita bila kukusalimia wakati mwingine hata kama anakufahamu. Wasomaji wanaweza kukubaliana na mimi kuwa wanawake wa aina hii wapo, hasa majumbani na maofisini.

Wanachangua watu wa kuongea nao, kusalimia nao. Ukiangalia anaojali kuwasalimia ni wale ambao yeye anaona wanaweza kumsaidia katika mambo yake tu.

Niwaambie tu watu wenye tabia hizi na hata wale dada zangu kuwa siku zote kiburi si maungwana. Aliimba hivyo Marijani Rajab katika wimbo wake, 'usia kwa watoto'.

"Nasisitiza heshima, heshima ni kitu cha bure, wanangu nisikilize, kiburi si maungwana, muwaheshimu wakubwa, pamoja na wadogo, tenda wema uende, usingoje shukurani aaa."

Maudhui ya wimbo huu ni baba akiwausia wanae, kuwa katika maisha heshima ni kitu cha bure, hakiuzwi madukani, akitaka wawaheshimu wakubwa na wadogo. Anawataka pia kutenda wema bila kusubiri shukurani. Ndiyo maana unaambia watendee hata wadogo ambao hawawezi kukulipa chochote. Ila hapo hapo kuna msemo unaosema 'wema hauozi.' Unaweza kufanya wema kwa mtoto mdogo leo, ikakaa akilini mwake, na akaja kukulipa hata baada ya miaka 30 wakati yeye ameshakuwa mkubwa na wewe kikongwe.

Ilitokea kwa kijana mmoja aliyewakuta watoto sita akiwa wamenunua vipakti vya biskuti kila mmoja, ila mmoja hakuwa nacho na alikuwa analia. Alipoulizwa akajibiwa na watoto kuwa wao walipewa na mama zao pesa, lakini mama yake hakuwa na pesa ya kumpa.

Kwa bahati mbaya hakuna hata mmoja aliyemjali kumpa. Kijana anamnunulia vipakti viwili vya biskuti. Kwanza akawa na vingi kuliko wenzake. Halafu hicho kitu mtoto yule alikiweka moyoni. Kijana aliona tu amefanya wajibu wake. Mtoto anakua na kila akimuona jamaa yule mtaani anakumbuka lile tukio. Miaka mingi ilipita, kijana akasoma na kuondoka nyumbani kwao.

Akiwa mzee anaumwa nyumbani kwake alijiwa na mgeni na akujitambulisha kuwa ni yule ambaye miaka mingi iliyopita alimnunulia vipakti vya biskuti. Mzee alikuwa amemsahau kwani aliondoka hapo miaka mingi na amekuwa mkubwa. Akamwambia kwa sasa ana maradhi mbalimbali ambayo yanahitaji gharama kubwa kutibika. Kijana yule ambaye awali alikuwa mtoto akamwambia asiwe na wasiwasi anamlipia mpaka ahakikishe amepona kwa sababu kitu alichokifanya hadi leo hakikutoka kwenye kichwa chake. Alisema wakati ule mama yake hakuwa na uwezo kabisa na baba yake alikuwa ameshafariki dunia.

Mbaraka Mwinshehe anasema katika wimbo wake, 'Uzuri si Hoja' anasema tabia njema ni silaha ya kupendwa popote.

"Hata uwe mzuri wa kupindukia, tabia yako ikiwa mbaya, watakufukuza, hata mwendo urembeshe, mithili ya twiga, bila maelewano mapenzi, hakuna kabisa, kuishi na wapo vyema hutoharibikiwa, milele na milele watakukumbuka.

Heshima kijana tambuliza kwanza mbele ujeuri mbaya ooo, uzuri si hoja, tambia njema ni silaha utapendwa popote oo." Tukitoka kwa Mbaraka tuje kwa Maximilian Bushoke, anakwambia 'Uzuri ni Tabia.'

"Uzuri si urembo utembezwao katika makapu, uzuri ni tabia ya pia ni maua," anasema katika wimbo huo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda.

Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka.

Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

# Aka Simtaki-7

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

Mzee Chilambo alionekana kubadilika. Hasira ilijidhihirisha machoni mwake. Akaona akiongea amekaa hatosikika. Akasimama na kuanza kupayuka "We mtoto, mimi baba yako au siyo baba yako? Niambie ukweli leo, labda mama yako amekwambia kuwa mimi si baba yako?" Akauliza kwa sauti kali na ya kitisho.

"Baba yangu." Akajibu Shani kwa sauti ndogo na ya woga. "Sasa kama mama yako kakwambia mimi ndiyo baba yako kwa nini hutaki kunisikia ninavyosema. Angalia, nyumba yetu ni ya udongo hii, japo ni ya bati, lakini unadhani ukiolewa sisi hatuwezi kujengewa nyumba ya matofali hapa? Tutakaa hivi mpaka lini?"

Shani hakujibu lolote, akaanza kutokwa machozi. Hayakumzuia mzee Chilambo kuendelea kufoka.

"We mtoto, unasema unampenda sana Shukuru wako huyo. Una kichaa. Siku hizi kuna mapenzi! Yaliondoka tangu enzi za nabii Nuhu na Safina yake. Siku hizi watu wanaangalia fursa! Wanakwenda kuishi sehemu ambayo anaona atafaidika, ataheshimika na kuonekana mtu mbele za watu. Hawabebwi tena na hisia za mapenzi. Hayo yaliwachelewesha hata bibi zetu enzi hizo. Siku hizi wanawake wanajitambua. Siyo kama wewe." Mzee Chilambo akazidi kubwata. Maneno hayo yalisababisha mkewe aingilie kati. "Basi baba Shani, usimwambie hivyo mtoto." "Nakwambia, nitawavuruga wote nyinyi wote wawili mtu na mama yake." Akasema huku akiwasogelea. Wote wakainamisha vichwa vyao na kuweka mikono juu yake ikiwa ni dalili ya woga. Akashika mikono ya binti yake, akaitoa kichwani. Akashika kichwa na kukitikitisa.

"We mtoto we mtoto..." Akashindwa kuongea maneno mengine kwa hasira aliyokuwa nayo. Akaendelea kumtikisa, mpaka Bi Hanifa alipoingia kati na kuzuia mtoto. "Muache bwana mtoto unamuumiza." "Ahaa kumbe wewe ndiyo unayemtia kiburi nimeshatambulia." "Mume wangu mtoto hataki huwezi kumlazimisha. Unaweza kumpeleka punda mtoni, lakini huwezi kumlazimisha kunywa maji." "Labda awe punda wa jirani, lakini kama wa kwangu atakunywa tu." Akajibu mzee Chilambo kwa hasira, akionekana anaweza kufanya kitu chochote kile kibaya wakati wowote ule. Wakati huo, Shani alikuwa amelala kwenye miguu ya mama yake kwa woga. Huku akilia kimya kimya. Kwa wakati huo hakuna mtu yeyote wa kumtetea zaidi ya mama yake tu. Ni yeye ndiye angeweza kumuokoa kwenye kipigo kutoka kwa baba yake.




**"Nakwambia we mwanaume ninamtaka mwanangu. Tena namtaka mzima wa afya. Asitudi mgonjwa wala maiti. Na akija maini utaila nyama namwambia." Ilikuwa ni sauti kali ya Bi Hanifa ikimbwatukia mumewe.**

***************************

"Sharifa hukuwepo malaika wako alikuwepo." "Eeeh! Unataka kuozeshwa mwanaume usiyemfahamu eee!" "He nimechoka mie hoi. Baba ndiye anayemtaka. Hataki kusikia lolote wala chochote." "He makubwa. Na Shukuru naye vipi?" "Mh! We acha tu shoga yangu." "Ina maana huyo mtu usiyemjua ndiyo kaleta barua?"

"Wote dada, wote wameleta. Unajua kulikuwa kama kuna tetesi hivi za kuletwa barua, nikamfuata haraha Shukuru nikamwambia awe na hela awe hana, alete barua haraka, ili zikikutana nyumbani mimi ndiyo niamue niolewe na nani. Nisingeweza kukataa, ingekuwa ngumu barua imekuja halafu unakataa, ningewambia sasa nataka kufanya nini nyumbani, wakati mtu wa kukuoa amepatikana. Shukuru akaleta. Badala ya mimi ndiyo nichague, baba na ndugu zake, pamoja na baadhi ya wajomba zangu wakaipiga chini ya Shukuru kwa sababu ilikuwa na pesa ndogo, sijui elfu tatu, sijui tano dada, lakini ile ya huyo wanayemtaka wao ilikuwa na shilingi elfu thelathini, akaipitisha." Yalikuwa ni mazungumzo kati ya Shani na shoga 'ke Sharifa, alipokwenda kumtembelea nyumbani kwake. Shani alifunga safari kwenda kwa Sharifa, siku mbili baada ya sekeseke alilolipata kutoka kwa baba yake.

"Kwani wa wapi huyo?" "Nasikia kijiji jirani cha Mtakuja, halafu nasikia ni maarufu, ni mtoto wa mzee Kibopa..." "Ahaaa nishamjua, Fotu huyo." "Eeeh! Ndiyo yeye huyo huyo. Ila mimi sijawahi hata kumuona."

"Sasa yeye amekuona wapi mpaka kaamua kuleta barua?" "Sijui, ila inawezekana yeye kuwa ameniona sehemu." Shani akajibu. "Wale kwao mambo safi." "Basi hilo baba ndiyo linamtoa roho, kaniambia mimi nitaolewa naye nitake nisitake, kisa wao ndiyo katika vijiji vyote vya huku Ugalla ndiyo wana mali." "Kwa nini asiwatafute matajiri wenzake kafuata wewe?" "Ndiyo hapo sasa shoga 'angu Sharifa nashangaa. Mimi Shukuru nitaanzia wapi kumuacha?" "He makubwa, ile wewe endelea na msimamo wako, ifike wakati wanawake sisi tusiyumbishwe. Yaani wanaume tu ndiyo wawe na uhuru wa kuchagua wachumba, ila sisi hatuna uhuru wa kuwakubali au kuwakataa. Tufanywe kama mazuzu tu, ambaye humtaki umkubali kwa lazima, na unayemtaka wazazi wanamkataa, naona hii ifike mwisho. "Yaani wewe hujui tu, mimi nimeshikilia msimamo wangu ule ule hata kama watamua." "Shikilia hapo hapo shoga 'angu, kama utajiri ni wao wenyewe, wewe unajua walipoupata." "Ndiyo maana nakupenda sana rafiki yangu.

********************************

"Nakwambia we mwanaume ninamtaka mwanangu. Tena namtaka mzima wa afya. Asitudi mgonjwa wala maiti. Na akija maini utaila nyama namwambia." Ilikuwa ni sauti kali ya Bi Hanifa ikimbwatukia mumewe.

Na hii ni baada ya kutoonekana kwa Shani. Kwa muda wa siku tatu hakuonekana nyumbani.

Wazazi wametafuta wapi! Majirani wamemsaka lakini hawajamuona.

"Atapatikana tu, huu mchezo unaocheza na mwanao mimi naujua. Yaani umekula njama na binti yako ili kunirusha mimi roho nikubali lengo lenu. Mimi sina hata presha, yupo mzima wa afya ni hii ni mipango tu, mnadhani mkifanya hivi ndiyo nitakubali aolewe na mwanaume hana elimu, mwizi tu hapa kijijini, anaibia watu mazao, maembe, korosho, hapana." Akajibu mzee Chilambo kwa kujiamini, alionekana hana wasiwasi wowote wa binti yake kupotea.

Kilichotokea ni kwamba baada ya kuona baba yake hataki anachokitaka, Shani alikusanya kilicho chake na kutokomea kijiji cha kijirani kiitwacho Ilembo. Baada ya giza kuingia alilazimika kulala kwenye vichaka. Ulikuwa ni usiku mrefu sana kwake, kwani hakupata lepe la ushingizi. Pamoja na woga alionao, lakini aliona ni bora kuliwa na wanyama wakali kuliko kuendelea kukaa nyumbani kwao kwa hali ile ya kulazimishwa kuolewa na mwanaume asiyempenda.

Salum na Dora, mtu na dada yake ambao walikuwa wanakwenda shamba alfajiri ndiyo waliomuona akiwa amelala usingizi mnono alioupata alfajiri.

Kwanza walidhani ni mtu aliyekufa. Wakaogopa kumsogelea, lakini Salum alihisi anapumua, akamsogelea mpaka alipo. Alipojidhihirisha kuwa yu hai, akamwamsha.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# 'UJANA' WA HARMONIZE KITENDAWILI

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Harmonize, bado analeta wasiwasi kuhusu ujio wa Remix ya wimbo wake wa Yanga Bingwa, baada ya awali kutofautiana na msanii kutoka DRC, Innoss B, ambaye alitaka kufanya kolabo ya wimbo huo.

Wiki kadhaa sasa, Harmonize, amekuwa akitangaza wimbo mpya unaoitwa Ujana, ambao unaonekana kuwa Remix ya wimbo huo, lakini bila sauti ya Innoss B.

Msanii huyo ameutambulisha wimbo huo kama mbadala wa "Yanga bingwa, official yanga anthem" uliotambulishwa wiki mbili zilizopita kuelekea siku ya Mwananchi Day iliyofanyika mapema mwezi huu katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Awali Innoss'B alikana kuhusika katika kuondoa toleo la kwanza la wimbo wa "Yanga Bingwa" katika mtandao wa You Tube, na hadi sasa hakuna taarifa zozote kuhusu ujio wa "remix" hiyo.

# OSU UMAARUFU KWAKE UNATOSHA

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Beverly Osu amekiri kuwa sasa anafurahi baada ya kushindwa aliposhiriki shindano la Big Brother Africa mwaka wa 2013.

Akizungumza hivi karibuni, Osu alifunguka kuwa awali alihisi uchungu kutupwa nje, lakini sasa amekuwa na furaha zaidi baada ya kupata umaarufu na njia ya kupata pesa kutokana na shindano hilo.

"Sasa naona kutoshinda kama baraka na nimefarijika kwa kushindwa kwani umaarufu niliopata unatosha," amesema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CRYSTAL YAIBANIA NEWCASTLE
CRYSTAL Palace inajiandaa kukataa ofa ya nne yenye thamani ya zaidi pauni milioni 65 kutoka kwa Newcastle ili kumuuza beki wa kati wa England, Marc Guehi, ambaye ana umri wa miaka 24. (**Sky Sports**), external

### CHALOBAH ANUKIA CHELSEA
CHELSEA inatajwa kuweka mipango imara kuhakikisha inamnasa beki raia wa England, Trevoh Chalobah, ambaye ana umri wa miaka 25 na pia anatakiwa na Kocha Mkuu wa Newcastle, Eddie Howe. (**Talksport**), external

### LACROIX KIMEELEWEKA
CRYSTAL Palace imefikia makubaliano binafsi na beki wa kati Mfaransa, Maxence Lacroix (24), ili kurahisisha mchakato wa kujiunga na Wolfsburg ya Ujerumani. (**Sky Germany - in German**), external

### MADUEKE HUYO NEWCASTLE
NEWCASTLE inajipanga kumsajili winga wa Chelsea, Noni Madueke, kwa dau la pauni milioni 30 lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 anatarajiwa kutua klabuni hapo kwa mkopo katika usajili wake wa awali. (**Football Insider**), external

### MERINO AJIPANGA KUONDOKA
MIKEL Merino anajiandaa kujiondoka katika kikosi cha Real Sociedad kitakachocheza mechi ya kwanza ya La Liga dhidi ya Rayo Vallecano leo huku akisubiria mchakato wake wa kuihama timu hiyo kukamilika, (**Guardian**)

### DYCHE, EVERTON KUTETA
KOCHA wa Everton, Sean Dyche, amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake na hadi sasa hakuna mazungumzo ya kusaini mkataba mpya lakini anaamini wataelewana na kubakia klabuni hapo(**Guardian**), external

### DELE ALLI MTEGONI EVERTON
KIUNGO raia wa England, Dele Alli, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru anatarajiwa kupewa mechi za majaribio ili kuthibitisha kiwango chake na mabosi wa Everton kabla ya kuamua kumpa mkataba nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. (**Guardian**)

### LINDELOF SOKONI ITALIA
BEKI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Sweden, Victor Lindelof, ambaye ana umri wa miaka 30 anawindwa na Fiorentina ya Italia. (**Gianluca Di Marzio - in Italian**).

### MEJBRI ATAKA UHAKIKA
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Tunisia, Hannibal Mejbri,atakuwa tayari kuondoka tu Manchester United baada ya kupata mkataba wa kudumu, huku Rangers na Celtic zote zimeonyesha nia ya kuhitaji huduma ya mkopo kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (**Football Insider)**

### ABRAHAM AITWA SAUDIA
NYOTA wa Roma, Tammy Abraham (26), anajiandaa kujiunga na timu moja inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudia ingawa West Ham tayari wameweka wazi wanamhitaji straika huyo raia wa England. (**La Repubblica - in Italian**).

### ALONSO AMTAKA TAH
KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, amesema beki wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Jonathan Tah, yuko katika mipango yake ingawa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 anatakiwa pia na Bayern Munich. (**Sky Sports Germany)**

### PSG YAMWANIA DOUE
PARIS St-Germain iko tayari kuipiku Chelsea katika mbio za kumsajili kiungo wa klabu ya Rennes ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 23, Desire Doue. (**ESPN)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CANCELO AHUSISHWA KUREJEA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

●●● Guardiola asifia kiwango cha nyota huyo na kuongeza muda utaamua...

PEP Guardiola amependekeza kunaweza kuwa na njia ya kurejea kwa nyota wake, João Cancelo, katika kikosi cha Manchester City.

Cancelo aliondoka kwa mshtuko Januari, mwaka 2023 na kwenda kujiunga na Bayern Munich kwa mkopo.

**Timu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani (Bundesliga), iliamua kutofanya uhamisho huo kuwa wa kudumu na msimu uliopita alikaa kwa mkopo Barcelona.**

Barcelona wanataka kumsajili tena Cancelo kwa mkopo, lakini kwa sasa beki huyo wa pembeni wa Ureno, ambaye hajaichezea City kwa miezi 18, amerejea mazoezini chini ya Guardiola.

"Anafanya mazoezi nasi," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Tutaona, labda tubaki, labda tuende kwa mkopo. Sijui bado. Anafanya mazoezi nasi, anatabia nzuri sana kwenye vipindi vya mazoezi. Anapenda kucheza mpira. Tutaona."

Alipoulizwa kama anaweza kuichezea City tena, Guardiola alisema: "Inaweza kutokea, ndio."

Cancelo ametajwa mara mbili katika timu bora ya mwaka ya Ligi Kuu (PFA) na alikuwa sehemu muhimu ya City kushinda taji mwaka wa 2021 na 2022.

Ana mkataba pale uwanja wa Etihad hadi 2027 na ingawa bado yuko tayari kwa uhamisho, hakuna uhakika.

"Katika mazoezi tunasalimiana na kuzungumza," alisema Guardiola.

"Kuhusu nini kitakachotokea inategemea na mawakala wake na klabu. Mwishoni, ikibidi abaki tutamchukulia kama wachezaji wengine wote kama tulivyofanya tangu nikiwa hapa.

"Kwa heshima, na kujaribu kuchukua kilicho bora zaidi kwa sifa zake kubwa alizonazo. Sina shaka na sifa zake kwa sekunde moja. Lakini sijui nini kitatokea."

Guardiola pia amekataa kuondoa uwezekano wa City kufanya usajili mwingine kabla ya tarehe ya mwisho baada ya kuwapoteza, Julián Álvarez na Oscar Bobb.

# ZIRKZEE NYOTA IMEWAKA UNITED

**MANCHESTER,** England



JOSHUA Zirkzee alisifia mwanzo mzuri wa Manchester United baada ya kutoka kwenye benchi na kufunga bao la ushindi dakika za lala salama walipocheza dhidi ya Fulham, hapo juzi.

United walishinda bao 1-0 katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu England uliochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford baada ya Mholanzi huyo kuingia akitokea benchi na kufunga dakika ya 87.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Zirkzee kuonekana katika kikosi cha United kufuatia uhamisho wake wa pauni milioni 36.5 kutoka Bologna msimu huu wa joto.

“Ni bora zaidi, sivyo?,” alisema Zirkzee akiiambiaBBC.

“Imekuwa nzuri sana tangu nilipofika,” aliongeza Zirkzee. “Kundi limekuwa la kushangaza, najisikia raha sana na nipo nyumbani hapa. Nina wakati mzuri sana.

“Kwa kweli ni klabu kubwa, lakini tunafanya kazi kwa bidii kila siku na kuzingatia kile tunachotaka kufikia, na hiyo ndiyo kuwa bora zaidi tunaweza kuwa. Kwa sasa sihisi shinikizo lolote.”

Ilionekana inaweza kuwa jioni ya kufadhaisha kwa United na Kocha, Erik ten Hag baada ya kukosa nafasi nyingi.

Bruno Fernandes na Mason Mount walizidisha nafasi kabla ya Zirkzee kuingia kama mchezaji wa akiba katika kipindi cha pili na hatimaye kutafuta njia ya kumpita kipa wa Fulham, Bernd Leno na kumalizia kwa ustadi mpira wa kona kutoka kwa Alejandro Garnacho.

“Ushindi huo unapendeza sana,” alisema Ten Hag akiiambia BBC.

“Kuanza msimu kwa ushindi siku zote ni muhimu. Hatuko tayari kama kikosi, kama timu, wachezaji wengi hawako fiti kabisa. Tulikuwa na siku 10 tu na timu hii kufanya mazoezi ya pamoja. Natarajia zaidi kutoka kwa timu hii, lakini tuna msingi tunaoweza kujenga juu yake.”

Ten Hag pia alifafanua kwa nini Jadon Sancho aliachwa nje ya kikosi cha siku ya mechi dhidi ya Fulham.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amejumuishwa tena baada ya kutofautiana na Ten Hag msimu uliopita na alishiriki kikamilifu katika ziara ya United ya kujiandaa na msimu mpya Marekani.

Lakini aliachwa nje ya kikosi juzi usiku huku Hag akifichua alikuwa ametatizwa na maambukizo ya sikio wakati wa maandalizi ya mchezo.

“Kwanza kabisa, tunahitaji kina kikosi,” alisema.

“Huu utakuwa msimu wa kunusurika kwa walio fiti zaidi na ninaweza kuweka wachezaji 20 tu kwenye kikosi. Jadon, katika wiki hiyo, alikuwa na ugonjwa wa sikio. Hakuwa fiti kwa asilimia 100.

“Angeweza kucheza, lakini mimi hufanya uchaguzi na kupendelea wachezaji wengine kwenye benchi,” ten Hag aliendelea. “Hiyo inaweza kubadilika na itabadilika msimu huu.

“Unaona jinsi wachezaji wa chini walivyo muhimu. Wakati mwingine inakatisha tamaa kwa mchezaji lakini inahusu timu, klabu. Tuna michezo mingi ya kucheza.”

# PSG waanza maisha safi bila Mbappe

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain ilianza enzi mpya bila Kylian Mbappé kwa kuifunga Le Havre mabao 4-1 kwenye mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Hata hivyo, matokeo yalikuwa mazuri zaidi kuliko kiwango kilichopendekezwa, huku mabao matatu ya mwisho ya PSG yakipatikana katika dakika tano za mwisho.



Klabu hiyo ya Paris imetawala soka ya Ufaransa ikiwa na mataji 10 ya ligi katika misimu 12 iliyopita lakini inajijenga upya baada ya Mbappé kuondoka na kujiunga na Real Madrid msimu wa joto.

Wana moja ya timu changa zaidi kwenye ligi msimu huu na wanaweka dau kuwa kizazi kipya kinaweza kuchukua jukumu zaidi baada ya Mbappé kuondoka.

“Haikuwa rahisi hata kidogo,” alisema bosi wa PSG, Luis Enrique akiwaambia waandishi wa habari kuhusu ushindi huo.

“Labda tulianza kwa utulivu sana. Tulifunga bao haraka sana na hilo lilitulegeza kidogo.”

Walianza mechi wakiwa na mchezaji wa nyumbani Ibrahim Mbaye mwenye umri wa miaka 16 kwenye winga ya kushoto na kuchukua uongozi baada ya dakika tatu pekee kutokana na bao la mshambuliaji wa Korea Kusini mwenye umri wa miaka 23, Lee Kang-in.

PSG walipata pigo wakati Gonçalo Ramos alipoumia kwenye changamoto na nafasi yake ikachukuliwa na Randal Kolo Muani dakika ya 20.

“Mimi si daktari lakini nadhani inaonekana kama jeraha baya sana. Sijui atakuwa nje kwa wiki ngapi,” alisema Luis Enrique.

Kolo Muani nusura afunge akigonga lango baada ya dakika 25, lakini bao la pili lilipopatikana lilikuwa upande wa pili.

Gautier Lloris, kaka yake mlinda mlango wa Ufaransa aliyeshinda Kombe la Dunia, Hugo, alisawazisha baada ya dakika 48 na uhakiki wa video pekee uliozuia wenyeji kuchukua uongozi baada ya Josué Casimir kupachika wavu dakika tano baadaye.

PSG walizidisha presha mechi ikiendelea lakini haikuwa hadi dakika ya 85 ambapo Ousmane Dembélé aliwafunga wageni kwa kichwa.

Bradley Barcola mwenye umri wa miaka 21 alipata la tatu dakika moja baadaye naye Kolo Muani akaongeza la nne kwa mkwaju wa penalti katika dakika ya mwisho ya mechi.

# Chelsea itasajili zaidi - Maresca

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Enzo Maresca, amesema klabu hiyo inalenga wachezaji wengine wanaoingia kabla ya mwisho wa dirisha la uhamisho licha ya kukamilisha usajili wa 10 wa majira ya kiangazi mapema wiki hii.

Pedro Neto alijiunga na Chelsea kwa kitita cha pauni milioni 54 kutoka Wolves Jumatatu iliyopita, akifuata Tosin Adarabioyo, Kiernan Dewsbury-Hall, Filip Jörgensen, Omari Kellyman, Aaron Anselmino, Caleb Wiley, Renato Veiga na Marc Guiu kutua London Magharibi.

Shughuli hiyo imeifanya Chelsea kubaki na kikosi cha wachezaji 43 ambao wanatazamia kuwauza wachezaji wasiotakiwa akiwamo, Conor Gallagher, ambaye pendekezo lake la uhamisho wa pauni milioni 34 kwenda Atlético Madrid limesitishwa huku klabu hiyo ya LaLiga ikipambana kukamilisha dili hilo.

Chelsea wapo kwenye mazungumzo na Atlético kuhusu uwezekano wa kumnunua João Félix huku Napoli wakiwa tayari kumjumuisha Victor Osimhen katika mpango wa kubadilishana wachezaji pamoja na fedha kwa Romelu Lukaku.



Alipoulizwa kuhusu Félix na Osimhen, Maresca alisema: “Kitu pekee ninachoweza kusema ni lazima niseme sawa kila wakati. Wao sio wachezaji wetu kwa hiyo si sahihi, nadhani, kuzungumzia mchezaji wa Napoli. au -- mwingine ni nani -- mchezaji wa Atlético Madrid.

“Kwa wakati huu, klabu inajua kile ninachofikiria kuhusu kile tunachohitaji ikiwa tutafanya kitu na tunatumaini kabla ya kumaliza dirisha la uhamisho, tunaweza kuleta wachezaji wengine.”

Gallagher na Trevor Chalobah ni miongoni mwa wachezaji kadhaa wanaofanya mazoezi mbali na kikosi cha kwanza.

Gallagher hatakuwepo dhidi ya City, wakati Ben Chilwell, Armando Broja na Raheem Sterling ni miongoni mwa wachezaji ambao wanaweza kuondoka kabla ya dirisha kufungwa.

“Tumekaa Marekani kwa siku 20 tukiwa na wachezaji 28, 29 kwa hiyo imekuwa nzuri katika kukisimamia kikosi,” alisema Maresca.

“Sasa tuna vijana ambao hawahusiki na kikosi chetu, wanafanya mazoezi tofauti, kwa sasa sio ngumu, pia kwa sababu nikianza kufikiria nina wachezaji 43, labda sio jambo zuri.”

HABARI MICHEZO

# SARE YA KWANZA LIGI KUU BAADA YA MISIMU MINNE

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25, ilianza kwa suluhu juzi wakati Pamba Jiji ikiwa nyumbani ilipolazimishwa matokeo hayo dhidi ya Prisons, ikiwa ni sare ya kwanza katika mechi za ufunguzi baada ya misimu minne.

Ikicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu baada ya miaka 23, Pamba Jiji ilijikuta ikishindwa kabisa kupata ushindi mbele ya mashabiki wake kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza na kuambulia kugawana pointi.

Mara ya mwisho mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika kwa sare ilikuwa ni msimu wa 2019/20, mechi ikichezwa Agosti 24, mwaka 2019 kwenye uwanja huo huo wa CCM Kirumba kati ya Mbao FC dhidi ya Alliance, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1, mabao yakifungwa na Paschal Liponda, huku beki wa Mbao Ibrahim Said akijifunga.

Misimu minne iliyofuata, mechi zote za ufunguzi ziltoa mshindi, Namungo ikiifunga Coastal Union bao 1-0, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Lindi, 2020/21, Mbeya Kwanza iliichapa Mtibwa bao 1-0, 2021/22, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro, Ruvu Shooting ikishinda bao 1-0, msimu wa 2022/23 dhidi ya Ihefu, Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, na msimu uliopita kwenye uwanja huo huo, Ihefu ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Geit Gold.

Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Goran Kopunovic, licha ya kutopata ushindi ameeleza kuridhishwa na kiwango cha wachezaji wake, akisema wengi wametoka kucheza Ligi ya Championship na wamecheza dhidi ya timu kongwe ya Ligi Kuu.

"Nimeridhika, hii ni timu mpya ambayo imepanda kutoka Ligi ya Championship, kiwango cha huko na Ligi Kuu ni tofauti, nawashukuru wachezaji wangu wamepambana na timu kongwe, yenye wachezaji wazuri ya Prisons," alisema kocha huyo raia wa Serbia.

Hata hivyo kocha huyo alilalamika kikosi chake kilikosa ushindi kutokana na kupangua kikosi muda mchache kabla ya mechi hiyo haijaanza.

Mserbia huyo alisema alilazimika kuwaondoa wachezaji wake watano waliokuwa katika kikosi cha kwanza baada ya kubainika usajili wao ulikuwa haujakamilika.

Naye Kocha Msaidizi, Shaaban Kazumba, alisema kwa kiasi kikubwa suluhu hiyo imepatikana kwa sababu ya kufahamiana.

Pamba Jiji wanamfahamu Kocha, Mbwana Makata kwa sababu aliifundisha timu yao, na yeye anaifahamu, hii imechangia sana, tulianza mechi ili tupate mabao ya mapema, tukapoteza nafasi nne za wazi, kipindi cha kwanza eneo letu la katikati halikuwa zuri ilibidi tufanye mabadiliko, kipindi cha pili pia tukatengeneza nafasi tukashinda kuzitumia, timu yetu ina mapungufu madogomadogo ambayo tunakwenda kuyarekebisha," alisema Kazumba.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 12 wakiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kwa ajili ya safari ya kuelekea China kushiriki mashindano ya vijana ya Female Universal Youth Cup yatakayofanyika kuanzia Agosti 21 hadi 23, mwaka huu nchini humo. **PICHA: TFF**

# Azam FC, APR hapatoshi Afrika

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Azam FC kinatarajia kuwakaribisha APR kutoka Rwanda katika mechi ya kwanza ya hatua ya awali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Azam FC, Bruno Ferry, alisema jana jijini mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu kila timu imejiandaa kusaka ushindi.

Ferry alisema amekiandaa vyema kikosi chake ili kuhakikisha wanaanza vizuri michuano hiyo na kujiweka katika nafasi salama ya kusonga mbele.

Alisema timu yake ilistahili kufuzu mashindano hayo na sasa wanachotaka kukionyesha ni ubora wao pia katika michuano hiyo ya kimataifa inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Michuano hii ni muhimu sana kwetu kwa sababu kama tupo hapa leo, basi ni kwa sababu tulifanya kazi kubwa msimu uliopita kuipata tiketi hii. Ilikuwa ni kazi kubwa kutoka kwa wachezaji, benchi la ufundi na watu wote wanaoizungumza timu, hivyo tunaweza kusema tumestahili kuwa hapa kucheza michuano hii," alisema Ferry.

Naye beki wa timu hiyo, Cheikh Sidibe, alisema wako tayari kwa mechi hiyo na wanatarajia kupata ushindi.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mechi hiyo na kila mechi iliyoko mbele yetu, tumejipanga na tuko tayari kwa ajili ya kupata ushindi katika mechi ya Jumapili, Inshaa-Allah tutashinda," alisema beki huyo.

## Boda boda Cup waaswa nidhamu

**Na Shufaa Lyimo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amewaasa washiriki wa mashindano ya bodaboda ya 'Arise and Shine Cup 2024' kudumisha nidhamu na kuwa na hofu ya Mungu.

Chalamila pia amewataka washiriki wa mashindano hayo kuwa na ushikamano ili kufanikisha shindano hilo ambalo linashirikisha timu 66 kutoka katika wilaya zote za Dar es Salaam.

"Pongezi kwa Boniface Mwamposa kwa kuandaa mashindano haya ambayo yatashirikisha vijana ambao ni maofisa usafirishaji (bodaboda) kutokana na kutambua thamani ya michezo hususani kwa upande wa vijana," alisema Chalamila.

Naye Mwamposa alisema lengo la mashindano hayo ni kuinuia vipaji vya vijana wa bodaboda ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya usafirishaji na kudai ataendelea na katika makundi mengine ya kijamii.

Alitaja zawadi kwa timu itakayoshika nafasi ya kwanza itapata zawadi ya boda boda tano wakati mshindi wa pili watapewa boda boda tatu na mshindi wa tatu watakabidhiwa boda boda mbili.

## Warriors Queens yachemka CECAFA

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Warriors Queens ya Zanzibar imejiondoka kushiriki mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki kwa Wanawake (CECAFA), kutokana na kukosa fedha za kuisafirisha timu hiyo kwenda Ethiopia.

Mashindano hayo yalianza rasmi jana na yatamalizika Agosti 31, mwaka huu ambapo bingwa ataiwakilisha CECAFA kwenye Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake.

Meneja Mashindano wa CECAFA, Yusuf Mossi, aliliambia gazeti hili Warriors Queens iliwasilisha taarifa za kujiondoa Alhamisi na wamelazimika kufanyia mabadiliko ratiba ya michuano hiyo.

"Bahati mbaya Warriors Queens wamejitoa katika mashindano haya Alhamisi usiku kutokana na changamoto za fedha. Sasa tumebakia na timu nane zitakazoshiriki michuano hii," Mossi alisema.

Simba Queens kutoka Tanzania Bara ilishawasili Ethiopia kwa ajili ya kushiriki michuano hiyo na itaanza kutupa karata yake ya kwanza kesho kwa kuvaana na FAD ya Djibouti kwenye Uwanja wa Abebe Bikila.

Michezo

Jumapili Agosti 18, 2024

Nipashe



Cancelo ahusishwa kurejea Man City UK. 21



Winga wa Yanga, Yao Kouassi (kushoto), akijipanga kumtoka beki wa Vital'O ya Burundi, Prince Michel Musore, katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yaanza safari kuwania taji Ligi Kuu

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

SAFARI ya matumaini ya wanachama, mashabiki, viongozi na wachezaji wa Simba kuurejesha ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara klabuni kwao baada ya kuukosa kwa misimu minne iliyopita inaanza leo watakapoikaribisha Tabora United kwenye Uwanja wa KMC, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, aliliambia gazeti hili jana anaamini timu yake itaibuka na ushindi ingawa haitakuwa mechi rahisi.

Fadlu alisema haifahamu vizuri Tabora United, lakini amekiandaa vyema kikosi chake kuibuka na ushindi katika mchezo wao huo wa kwanza msimu huu.

"Mechi za kirafiki na Ngao ya Jamii zimetujenga, lakini zimetupa somo na kujua nini cha kufanya, sasa tunakwenda katika mechi za ushindani. Hatuifahamu vizuri timu hii (Tabora United), inachezaje, lakini tunaamini maandalizi yetu yatatusaidia. Katika soka lolote linaweza kutokea, tunakwenda kucheza na timu nzuri lakini tunajiamini tutaibuka na ushindi," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

Naye Kocha Mkuu wa Tabora United, Francis Kimanzi, alisema wataingia katika mechi hiyo wakiiheshimu Simba kwa sababu ni moja kati ya timu kubwa si Tanzania tu, bali barani Afrika.

"Kwanza kabisa ni lazima tuwaheshimu kwa sababu ni timu kubwa, inahitaji matokeo mazuri na huwa inayapata kila mara, hii itakuwa ni kipimo kizuri kwa timu yangu ya Tabora United. Tunajua hatukuwa na wakati mzuri msimu uliopita, tunajaribu kupandisha morali ya wachezaji waliokuwepo msimu uliopita, pia watu wakumbuke sasa timu hii ina wachezaji wengine wapya na benchi jipya la ufundi," alisema Mkenya huyo.

Simba imesajili wachezaji wapya 14, tisa wa kigeni na watano wazawa, hii baada ya kupitisha 'fagio' katika kikosi chake, nyota hao wapya ni Moussa Camara, Joshua Mutale, Steven Mukwala, Jean Charles Ahoa, Debora Fernandes Mavambo, Augustine Okajepha, Valentin Nouma, Karaboue Chamou, Lionel Ateba, Omari Omari, Abdulrazack Hamza, Valentino Mashaka, Kelvin Kijili na Yusuph Kagoma.

Msimu uliopita, Simba ilivuna pointi sita kwa Tabora United, ikishinda mabao 4-0 ugenini kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora na kupata magoli 2-0 walipokutana kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

# YANGA YATAKATA MICHUANO CAF

### ●●● Yalamba Sh. milioni 20 za 'Goli la Mama Samia', usajili mpya walipa...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na wachezaji wapya, Prince Dube na Clatous Chama, huku mengine yakipachikwa na Clement Mzize na Stephane Aziz Ki, yameifanya Yanga kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kupata ushindi wa magoli 4-0 dhidi ya wenyeji, Vital'O ya Burundi.

Kwa ushindi huo, mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga walikabidhiwa kitita cha Sh. milioni 20, kila goli likiwa na thamani ya Sh. milioni tano, ambazo zitakuwa zinatolewa katika kila mechi ya kimataifa na Rais, Samia Suluhu Hassan.

Dube alisajiliwa na Yanga akitokea Azam FC baada ya kuvunja mkataba wake huku Mzambia Chama kutoka kwa Simba alitua kama mchezaji huru kutokana na kumaliza mkataba wake na Wekundu wa Msimbazi.

Iliwachukua Yanga dakika tano kupachika bao la kwanza katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ambapo kikanuni ilikuwa inacheza ugenini.

Bao hilo la Dube lilidumu mpaka timu hizo zilipokwenda mapumziko, lakini wenyeji Vital'O walikuwa wa kwanza kufika katika lango la Yanga kwa shambulio jepesi lililookolewa na nahodha, Bakari Mwamnyeto.

**Alikuwa ni Nickson Kibabage aliyepelekewa pasi ndefu katika wingi ya kushoto, akabaki na kipa wa Vital'O, Hussein Ndayishimiye, lakini shuti lake la mguu wa kushoto lilitoka nje kidogo ya lango.**

Dakika moja baadaye, Yanga ilifanya shambulizi lililofanana na hilo lililoipatia bao, Aziz Ki kwa mara nyingine aliuinua mpira mrefu wingi la kushoto uliomkuta, Dube eneo lile lile alilokuwepo Kibabage mwanzo, mwenzake hakufanya makosa, kwa mguu wa kushoto akaukwamisha wavuni dakika ya tano ya mchezo huo.

Baada ya bao hilo, Vital'O walionekana kuamka na kuamua kwenda mbele, lakini kwa mahesabu makali kwa sababu wanapopoteza mpira walikuwa wanarudi wengi langoni mwao.

Chama aliupata mpira akiwa katika eneo zuri, lakini shuti lake liliwababatiza mabeki wa timu pinzani dakika ya 18 na dakika ya 24 na 25, Vital'O walifanya mashambulizi langoni shuti la Fred Niyozideye lilipaa juu huku lile la Jean Nzeyimana, likiishia mikononi mwa kipa, Djigui Diarra.

Nusura Mwamnyeto aiandikie Yanga bao la pili dakika ya 35, aliporuka juu kuunganisha mpira wa kona uliopigwa na Aziz Ki, lakini uliondolewa kwenye mstari na beki Mrundi, Prince Musore.

Chama alipachika bao la pili dakika ya 68, baada ya kutokea piga nikupige langoni mwa Vital'O, baada ya shuti lililopigwa na Aziz Ki kugonga nguzo ya lango na kumfikia mfungaji aliyeukwamisha wavuni kirahisi.

Baada ya bao hilo, Chama alitoka na nafasi yake kuchukuliwa na Kennedy Musonda, mfungaji wa bao la kwanza, Dube naye akitoka na kuingia Mzize ambaye muda mchache baadaye akapachika bao la tatu.

Ilikuwa ni dakika ya 73, wakati mabeki wa Vital'O walipokuwa wakiuchezea mpira nyuma, mmoja akajaribu kumrudishia kipa, lakini kwa kasi, Mzize aliukimbilia na kumfanya kipa, Ndayishimiye aliyefanya kazi kubwa jana, kutokea, lakini alichelewa na hivyo kuifungia timu yake goli la tatu.

Aziz Ki, baada ya kosa kosa nyingi alifunga bao la penalti dakika ya 90 na kuifanya Yanga kuhitaji sare yoyote au kutofungwa idadi ya mabao zaidi ya manne katika mchezo wa marudiano utakaofanyika, Agosti 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mshindi wa jumla wa mechi ya Yanga dhidi ya Vital'O, anatarajiwa kukutana na mshindi kati ya CBE ya Ethiopia au SC Villa ya Uganda.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >